# Nipashe

Jumatano Februari 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581593

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**BILIONI** 988/- kuleta lami Km 250, masoko 18, stendi tisa Dar

UKURASA 5

**KISA MGANGA JADI** 16 wa familia moja wakutwa mahututi madai kunywa sumu

UKURASA 4

**MABADILIKO** yaja, Shule ya Sheria kusukwa upya

UKURASA 7



**PROFESA JANABI: SITII HOFU, SITANII**

UKURASA 5



**POLISI** waingilia kati, mvua yavunja mkutano ...

Uk. 2

# Lissu na Biteko watunishiana kugombea njia



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (kofia nyekundu), akiwaongoza wanachama na wafuasi wa chama hicho, kwenye maandamano ya amani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya jana. Kulia kwake ni Katibu Mkuu mstaafu wa CHADEMA, Dk. Wilbroad Slaa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

**MAZUNGUMZO MAALUM**

## Mjane wa 'nyama ya swala' afunguka siku 105 gerezani

**ALIKUSUDIA** kujiua, akaahirisha...*ukurasa 3*



Mjane Maria Ngoda

## Kilicho nyuma ya pazia vyuo vikuu maarufu nchini kushuka ubora

UKURASA 2

**MICHEZO** **AZAM YAANIKA SIRI KUIFUNGA** UK. 23

**KATUNI** UK. 6



Mkuu wa Idara ya Magari wa Chuo cha Ufundi Arusha, David Mtunguja (kushoto), akionyesha mitambo ya magari ya kujifunzia wanafunzi wa chuo hicho, kwa maofisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, baada ya kupatiwa mafunzo ya ukaguzi wa magari kwa kutumia vifaa vya kisasa zaidi jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Lissu, Biteko watunishiana misuli kugombea barabara

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

ALIMANUSURA vurugu zitokee jana kwenye maandamano ya amani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) baada ya msafara wa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, kuingiliana na ule wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

Vurugu hizo nusura zitokee eneo la Sae jijini Mbeya wakati waandamanaji walipokuwa katika barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) wakitokea Uyole kwenda kwenye uwanja ulioandaliwa kwa ajili ya mkutano wa hadhara, Ruanda Nzovwe.

Wakiwa katika maandamano huku wakiimba nyimbo za hamasa, nyuma yao ulitokea msafara wa Dk. Biteko ambaye alikuwa anatokea kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani Rungwe.

Askari waliokuwa wanaongoza msafara wa Biteko, waliamuru waandamanaji kupisha barabara ili upite kwanza hali ambayo ilizua kutoelewana baina ya pande hizo mbili.

Kutokana na hali hiyo, Lissu aliwataka wafuasi kuendelea na maandamano huku akiwataka askari waliokuwa wanaongoza msafara wa Biteko kupita njia nyingine au waendelee kufuata nyuma ya waandamanaji.

Alisema jana wao ndio waliokuwa na kibali cha kuitumia barabara hiyo na kwamba hakukuwa na taarifa zozote za kiongozi mwingine kuitumia kwa wakati huo.

"Waandamanaji naomba tuendelee na maandamano kwa mwendo ambao tumetoka nao. Gari yoyote ambayo inashiriki maandamano ije nyuma yetu lakini hatupishi mtu yeyote. Polisi ambao mnaoongoza huo msafara tafuteni njia nyingine," alisema.

Baada ya maelezo hayo, askari waliokuwa wanaongoza msafara wa Naibu Waziri Mkuu Biteko walielekeza magari ya msafara kupita kwenye barabara ya vumbi, hivyo kuruhusu waandamanaji kuendelea na safari.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini kupitia CHADEMA, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, alisema lengo la polisi waliokuwa wanaongoza msafara walitaka kuwagonga waandamanaji.

Alisema Biteko alitakiwa autumie mkutano huo wa hadhara kuwaeleza wananchi waliokuwa wamekusanyika kuhusu namna ambavyo amejipanga kutatua kero ya umeme kutokana na kukatika mara kwa mara.

Sugu alisema wananchi wamekuwa wakipata shida kwa kushindwa kufanya shughuli za maendeleo kutokana na uhaba wa umeme, hivyo akamtaka kuwaeleza wananchi ukweli.

"Sisi tumeandamana kwa lengo la kufikisha serikalini kero ambazo zinatukabili lakini Naibu Waziri Mkuu badala ya kutusikiliza, anataka kutugonga na gari. Watanzania wanachotaka ni kupunguziwa gharama za maisha," alisema Sugu.

Viongozi, wanachama wa CHADEMA pamoja na wananchi kutoka mikoa ya Kanda ya Nyasa waliandamana kwenye misafara mitatu tofauti. Msafara wa kwanza wa maandamano ya kilomita 18, uliongozwa na Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, kuanzia Mbalizi, msafara wa pili ukiongozwa na Lissu ulianzia Uyole na mwingine uliokuwa unaongozwa na Katibu Mkuu, John Mnyika, ulianzia Isanga.

**MVUA YAVUNJA MKUTANO**

Baada ya kutamatika kwa maandamano, kulifuatia mkutano wa hadhara uliopangwa kufanyika uwanja wa Ruanda, Nzovwe, lakini ulivunjika baada ya mvua kubwa kuanza kunyesha. Mvua hiyo ilianza kunyesha saa 10:08 jioni.

Baada ya maandamano hayo kufika kwenye uwanja huo, viongozi walijipanga kwa ajili ya kuanza kuhutubia. Walianza viongozi wa dini kuomba dua na sala.

Wakati viongozi hao wakijiandaa kuhutubia, iliibuka mvua ambayo iliambatana na upepo na kusababisha wananchi kwenda kujificha kwenye makazi ya watu jirani na uwanja huo. Baada ya mvua hiyo kuzidi, viongozi walipanda magari na kuondoka uwanjani.

**MABANGO**

Waandamanaji walikuwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali ambao ulikuwa unaelezea kero mbalimbali zinazowakabili ikiwamo ukali wa maisha.

Baadhi ya mabango yalikuwa na ujumbe unaosema 'Umeme umekuwa kero, tunashindwa kufanya kazi,' mabomba tunayo, bili ziko juu ila maji hayatoki', 'Kikokotoo kinatuhusu na sisi,' 'Tunataka Katiba Mpya,' 'Tunamtaka Rais asisaini miswada ya uchaguzi iliyopitishwa na bunge'.

Mabango mengine yalisema 'Gharama za maisha ziko juu, sukari bei juu, mafuta yanapanda kila siku' na 'tunataka bandari yetu'.

# Kilicho nyuma ya pazia vyuo vikuu maarufu kushuka ubora

**Na Restuta James**

UPUNGUFU wa wanataaluma, kukosekana fedha za utafiti, kusitisha ajira za wataalamu vyuoni pamoja na wingi wa wanafunzi wanaodahiliwa vyuo vikuu wasiolingana na miundombinu, vimetakwa kuwa chanzo cha kudorora elimu ya juu nchini.

Hayo ni maoni ya baadhi ya wadau wa elimu baada ya ripoti ya upimaji viwango vyuo vikuu Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuonyesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambacho ni kikongwe nchini, kuporomoka hadi nafasi ya 21 kutoka kwenye 10 bora.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, vyuo 10 bora katika ukanda huo na nchi kwenye mabano ni vinne (Afrika Kusini), viwili (Tanzania) huku nchi za Uganda, Rwanda, Nigeria na Ghana vikiwa na chuo kimoja kila moja.

Wakati UDSM ikionekana kuporomoka kwa ubora, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) vimevyoingia kwenye vyuo vikuu 10 bora.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wasomi wamechambua chanzo cha kuporomoka viwango na ubora wa vyuo nchini.

Dk. Peter Kafumu, mwalimu wa chuo na mtumishi wa umma, alisema ukosefu wa maprofesa ni sababu kubwa inayoporomosha ubora wa elimu ya vyuo nchini. Alisema vyuo vikuu vingi vya umma na binafsi havina wanataaluma (wahadhiri na maprofesa) kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema vyuo hivyo vinakosa maprofesa wabobezi na hakuna programu ya kuwaandaa warithi wa taaluma zao ili kuchukua nafasi baada ya kustaafu au kuondoka.

"Nimesoma chuo kikuu Ubelgiiji, nilishuhudia profesa mmoja awe wa jiolojia au kemia ana wasaidizi wawili ambao ni wahadhiri ili anapoondoka awe ameshiriki kuwaandaa warithi ambao pia wanapanda ngazi na kuziba nafasi yake," alisema.

Akirejea hali ya vyuo, alisema maprofesa wengi wamestaafu na hakuna wengine wa kuwarithi na kwamba ndicho chanzo cha kuporomoka kwa ubora.

Dk. Kafumu alisema ufumbuzi wa tatizo hilo ni kuwa na programu ya kuandaa na kurithisha ujuzi na utaalamu wenye utaalaamu, viwango na ujuzi watakaochukua nafasi za wabobezi wanapostaafu.

Mhadhiri mstaafu wa MUHAS, Dk. Eva Marie Semakafu, alisema tatizo ni utaratibu wa kuandaa wahadhiri wa vyuo vikuu kwa kuangalia ufaulu wa juu (GPA) kwa kumpa ajira aliyepasi sana badala ya kuangalia ubobevu na umahiri wa mwanafunzi tangu anapojiunga na chuo kwenye somo analotakiwa kulifundisha.

Alisema inawezekana mwanachuo akafaulu kwa alama A zote lakini hana sifa za kuwa mhadhiri wala kufundisha chuo si ndoto yake.

Dk. Semakafu alisema kuna haja ya kuangalia taratibu za kuandaa wanataaluma katika vyuo kwa vigezo vinavyotumika siku zote badala ya kutegemea GPA kubwa.

Pia alisema serikali kusitisha ajira za wanataaluma vyuo vikuu kwa muda mrefu imesababisha ombwe kwenye ngazi mbalimbali kuanzia wanaochipukia, waandamizi hadi wabobezi. Hali hiyo, alisema imesababisha upungufu mkubwa wa maprofesa hasa pale ambapo profesa anapostaafu kwa vile anakosa mrithi.

Mwanataaluma huyo mstaafu alisema wingi wa wanafunzi vyuoni hauendani na uwiano wa wanataaluma huku pia akibainisha kuwa miundombinu pia haitoshi katika vyuo vikuu vya umma na binafsi.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema japo hafahamu vigezo wanavyotumia kupima ubora wa vyuo vikuu, aligusia wingi wa wanavyuo kuwa ni mzigo kwa ufanisi.

"Mambo ya kuangalia ni pamoja na kudahili wanafunzi wengi wakati hakuna miundombinu, wahadhiri, maprofesa, mafunzo kwa vitendo, teknolojia ya kisasa na maktaba kuwezesha kupata elimu yenye ubora," alisema.

Alisema ufumbuzi wa tatizo hilo ni kufikiria na kutekeleza sera mpya ya elimu inayotaka wanafunzi kupata ujuzi na elimu ya ufundi katika vyuo vya kati vya awali badala ya wote kwenda vyuo vikuu.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Dk. Kaanaeli Kaale, alikumbusha kuwa viwango hivyo hupimwa kwa kutazama idadi na ubora wa machapisho ya wahadhiri na maprofesa wa vyuo vikuu ambayo huandikwa kwenye majarida ya kimataifa na kuangaliwa jinsi yanavyoongeza thamani na ubora kwenye elimu.

Alisema ukosefu wa wahadhiri na maprofesa umetokana na vyuo vingi vya umma kutokuajiri kwa kuwa serikali ilisitisha ajira zao na kuongeza ombwe linaloshusha ubora wa elimu ya juu.

Nafasi ya kwanza na ya pili inashikiliwa na Witwatersrand, Johannesburg mtawalia (Afrika Kusini), MUHAS, Pretoria (Afrika Kusini), Makerere (Uganda), Western Cape (Afrika Kusini), Covenant (Nigeria), UGHE (Rwanda), Ashesi (Ghana) na Ardhi (Tanzania).

HABARI KITAIFA

## Kilo milioni 1.96 dawa za kulevya zakamatwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imekamata kilogramu milioni 1.96 za mihadarati na watuhumiwa 10,522 huku wanaume wakiongoza kujihusisha na biashara hiyo haramu.

Watu walikamatwa wakiwa na dawa hizo katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mamlaka hiyo kwa kipindi hicho.

Alisema kati ya watuhumiwa hao waliokamatwa wanaume ni 9,701 na wanawake ni 821 na kwamba ekari 2,924 za mashamba ya bangi na mirungi ziliteketezwa kwa kipindi hicho.

"Kiasi cha dawa za kulevya kilichokamatwa katika kipindi cha mwaka mmoja pekee ni kikubwa zaidi kuwahi kukamatwa hapa nchini kwani kinazidi kiasi cha kilogramu 660,465 zilichokamatwa katika kipindi cha miaka 11," alisema.

Pia alisema serikali imezuia uingizaji wa kilogramu 157,738.55 za kemikali bashirifu ambazo zingeweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya kinyume cha sheria.

Alibainisha kuwa katika kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya tatizo la dawa za kulevya, serikali imepanua wigo wa utoaji elimu kwa kuelekeza nguvu kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo.

"Utafiti unaonyesha kwamba matumizi ya dawa yanaanza katika umri mdogo kati ya miaka 10 na 12. Hivyo, serikali imeona iweke mkazo huko kwani watoto wengi wanapitia katika shule hizo," alisisitiza.

Alisema elimu imeendelea kutolewa kwenye makundi mbalimbali ya kijamii yakiwamo ya viongozi wa dini, viongozi wa kimila, waandishi wa habari, vyombo vya ulinzi na usalama, maofisa forodha na wakulima hasa katika maeneo yaliyokithiri kwa kilimo cha bangi na mirungi.

Kadhalika, alisema elimu ya dawa za kulevya imeendelea kutolewa kupita vyombo vya habari, makongamano na maonesho ya kitaifa na kimataifa.

Kuhusu tiba, alisema serikali imeendelea kuimarisha huduma kwa kuongeza vituo vya kutolea tiba kwa waraibu kwa kutumia dawa na huduma za unasihi (MAT) na kwa mwaka 2023 kituo kimoja kilifunguliwa mkoani Morogoro katika Gereza la Kihonda ambapo hadi kufikia Desemba, mwaka jana, vituo 16 vilikuwa vinatoa huduma kwa walengwa.

Pia alisema vituo vingine viwili katika wilaya za Muheza (Tanga) na Chalinze (Pwani) vinatarajia kukamilika ifikapo Aprili, mwaka huu. Vituo vingine vitatu vitaanza kujengwa katika mikoa ya Shinyanga, Kilimanjaro na Pwani (Mkuranga).

Alisema serikali ipo kwenye hatua za mwisho za ujenzi wa kituo kikubwa cha huduma za tiba na utengamao katika Jiji la Dodoma ambacho mbali na huduma za matibabu pia yatatolewa mafunzo maalumu yatakayowawezesha waraibu kujitegemea kimaisha baada ya kukamilisha safari ya matibabu yao.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na ongezeko la waraibu wanaojiunga na tiba katika kliniki mbalimbali nchini.

"Sababu ya ongezeko hilo ni kuadimika kwa dawa za kulevya mtaani baada ya kuvunja baadhi ya mitandao mikubwa ya wauzaji wa dawa za kulevya. Takwimu kutoka kwenye vituo vya MAT zinaonyesha waraibu wapya 2,219 wamejiunga na tiba kwa mwaka 2023 na kufanya idadi ya wanaopata tiba ya Methadone kufikia 15,915," alisema Mhagama.

MAZUNGUMZO MAALUM

# Mjane wa 'nyama ya swala afunguka siku 105 gerezani

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MJANE Maria Ngoda alikusudia kujiua gerezani baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 22 jela mwishoni mwa mwaka jana.

Novemba 3, mwaka jana, mkazi huyo wa Isakalilo, wilayani Iringa, alihukumiwa kifungo hicho na Hakimu Mkuu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Said Mkasiwa baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe jana, Maria, alisema uamuzi wake awali baada ya kuhukumiwa kutumikia kifungo hicho ulikuwa kujiua akiwa gerezani.

Hata hivyo, kusudio lake hilo halikutimia baada ya faraja aliyopata toka kwa wafungwa wenzake pamoja na askari wa Jeshi la Magereza.

"Uamuzi huo (kusudio la kujiua) ulinitoka kabisa na furaha kubwa ilinijia baada ya kupata faraja gerezani.

"Sikuamini macho na masikio yangu kuona ninahukumiwa kwenda jela miaka 22 wakati siku ninakamatwa na kusingiziwa kesi hii ya nyama ya swala, niliambiwa nisiwe na hofu. Nitakapofika mahakamani nikubali kosa kwani sina hatia, bali ni shahidi wa Jamhuri.

"Ndio sababu nikakiri kosa baada ya kufika mahakamani, ni kutokana na maelekezo niliyopata toka kwao wenyewe (Upande wa Jamhuri) kuwa nikubali, nitaachiwa, kumbe haikuwa hivyo! Kwa kweli niliumia sana," alisimulia Maria.

Aliendelea: "Kwa kweli siku ile niliyohukumiwa (kifungo cha) miaka 22 nilijikuta ninakuwa na uamuzi mgumu na shetani alijiinua sana.

"Baada ya kufika gerezani siku ya kwanza kuanza kutumikia kifungo sikuwa na akiba ya vidonge aina yoyote na paa la gereza na madirisha yalikuwa juu sana sikuweza kufikia ila kama ningefikia na kungekuwa na kamba, nilikuwa mtu wa kufanya uamuzi mgumu zaidi.

"Yawezekana leo ingebaki stori, ila ninajua yalikuwa mapito na Mungu alitaka kusema nami kupitia hukumu ile na leo amenifanya Maria kuwa mtu wa tofauti ninayejulikana kila kona. Hakika, ninasifu wema na ukuu wa Mungu!"

Maria alisema kuwa akiwa gerezani, wakati wote alikuwa anatenga dakika 45 hadi 50 kusali na wakati mwingine alipokuwa katika maombi, "alipokea ujumbe ukimtaka asiogope hukumu hiyo".

"Nikimaliza kusali nilikaa pembeni na kuimba wimbo nilioupenda, ni wimbo wa lugha ya Kihehe unaosema 'watoto umewaacha na nani Maria?' Ni wimbo ambao uliinifikirisha na kujikuta ninatokwa na machozi, nikikumbuka watoto wangu hasa yule mdogo mwanafunzi ambaye alishindwa kuendelea na masomo wakati nikiwa mahabusu," alisimulia Maria huku akitokwa machozi.

***USIKOSE KESHO MWENDELEZO WA MAZUNGUMZO HAYA**



Mjane Maria Ngoda (katikati), akihojiwa na mwandishi wa gazeti hili, Francis Godwin nyumbani kwake, Isakalilo mjini Iringa jana. **PICHA: DISHON LINUS**

## Nondo ajitosa uenyekiti Ngome ya Vijana ya ACT

**Na Halfani Chusi**

MCHAKATO wa uchaguzi ndani ya Chama cha ACT-Wazalendo unazidi kunoga. Makamu Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya chama hicho, Abdul Nondo amechukua fomu kuwania uenyekiti wa ngome hiyo.

Nondo ametamba kuwa akichaguliwa katika nafasi hiyo, ataendelea kutetea maslahi na madai ya vijana serikalini na kwenye vikao vya uamuzi vya chama.

Aliyasema hayo jana kwenye ofisi za makao makuu ya chama hicho, Magomeni, mkoani Dar es Salaam muda mfupi baada ya kuchukua fomu kuwania nafasi hiyo.

Alitaja vipaumbele vyake saba atakavyoanza navyo, ambavyo ni pamoja na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo na ujasiri wa kiuongozi kwa viongozi wote waliochaguliwa nchi nzima na kutanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuimarisha ujenzi wa ngome kote nchini.

Nondo pia alisema ataendelea kudumisha na kuimarisha zaidi mtandao wa ngome kote nchini na kufanya ziara mara kwa mara.

Vipaumbele vingine ni kutanua na kuimarisha zaidi mtandao wa matawi ya ACT-Wazalendo vyuo vikuu nchini, kuhamasisha vijana kujitokeza kugombea, kupiga kura na kulinda ushindi katika uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025 pamoja na kutanua ngome kwa kufungua matawi nje ya nchi.

"Demokrasia ni miongoni mwa misingi muhimu sana inayoaminiwa na chama chetu kwa mujibu wa ibara ya 6(1)(vii) ya katiba yetu ya chama, toleo la 2020.

"Mwaka 2020 wakati ninaomba ridhaa kwenu kuwa Makamu Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana Taifa, hali ya demokrasia nchini ilikuwa mbaya sana; kutekwa kwa watu, mikutano kuzuiwa, vitisho na hofu ilikuwa sehemu ya maisha yetu.

"Katika kipindi hicho watu wengi waliogopa kuongea na kukosoa ila Ngome ya vijana ACT-Wazalendo hatukuogopa kuongea, kukosoa na kupinga vitendo vyote vya serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kuminya, kukanyaga na kutomasa demokrasia," alisema.

Nondo alikumbushia kuwa alisimama imara katika kulinda demokrasia, uhuru wa kuongea, uhuru wa vyombo vya habari, kudai mabadiliko ya sheria na Katiba mpya ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

"Huu umekuwa wajibu wetu wa kila siku kwenye utumishi wetu ndani ya ngome jana, leo na hata kesho kwa sababu demokrasia ndiyo nyenzo muhimu ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii," alisema Nondo.

Mgombea Mwenza, Nassor Ahmed Marhun ambaye kama akishinda atakuwa Makamu Mwenyekiti Zanzibar, alidai walishinda uchaguzi wa mwaka 2020, hivyo atahakikisha hakuna ukandamizaji demokrasia katika uchaguzi ujao ambao anaamini wagombea wa chama chao watashinda kwa kishindo.

"Tunawaahidi vijana wenzangu, mkituchagua tumejipanga kwa uchaguzi wa 2025, kutafuta ushindi, kulinda na kuutetea kama vijana wa taifa hili katika misingi stahiki ya nchi yetu, hatutokubali kuona ubakwaji demokrasia katika nchi yetu, tutasimama imara kutetea nchi yetu na haki za vijana kwa ujumla," alitamba.

Uchaguzi wa viongozi kwa nafasi wanazowania wawili hao umepangwa kufanyika Februari 28, mwaka huu.

KISA MGANGA WA KIENYEJI

# 16 wa familia moja wakutwa wakiwa mahututi nyumbani

**Na Maulid Mmbaga**

WATU 16 wa familia moja, wakazi wa Vijibweni, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, wamekutwa wakiwa mahututi nyumbani kwao baada ya kunyweshwa dawa inayodhaniwa kuwa ni sumu na mtu aliyejidai ni mganga wa kienyeji.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari jijini jana, akisema tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita saa tatu usiku.

Alisema mtu huyo alifika nyumbani kwa familia ya Mzee Halisi Amani kwa lengo la kutoa matibabu kwa mke wake, Fatuma Abdalla (52) aliyekuwa anasumbuliwa na maradhi ya miguu.

Kamanda Muliro alisema kuwa mtu huyo ambaye jina lake hakutaka kuliweka wazi kwa sababu za kiuchunguzi, aliwanywesha dawa iliyolewesha familia nzima, wakapoteza fahamu na akaiba simu tano za mkononi na kukimbilia kusikojulikana.

"Jeshi la Polisi linamtafuta mganga huyo na lazima tutamkamata. Pia limemkamata kwa mahojiano mtu mmoja anayefahamika kwa jina la Jalala Said anayedaiwa kushirikiana na mganga huyo.

"Wagojwa walilazwa na kupatiwa matibabu kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni. Mpaka sasa (jana saa nne asubuhi) wagonjwa 13 wameshapewa rukhsa kutoka hospitalini na wengine watatu wanaendelea kupatiwa matibabu na hali zao zinaendelea vizuri," Kamanda Muliro alisema.

Aliongeza kuwa tukio lingine kama hilo lilitokea Februari 9, mwaka huu huko Tuangoma, Mbagala, Dar es Salaam, mtu aliyejifanya mganga wa jadi aliwanywesha dawa zilizowalevya watu watano ambao walipoteza fahamu na kuwaibia pikipiki yenye namba za usajili MC474, simu tatu na Sh. 30,000.

Kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi linatoa hadhari kwa wananchi dhidi ya kuwapo watu hao wanaojifanya waganga wa jadi wanaosikiliza matatizo ya wanafamilia, hasa yanayohusiana na magonjwa ambayo yamedumu kwa muda mrefu na kutumia mwanya huo kuwanywesha dawa na kuwaibia.

"Tuwe nao makini na mkipata taarifa zozote za watu wanaotiliwa shaka, toeni taarifa hizo mapema, polisi wawahoji na tukibaini si waganga wa jadi tutachukua hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani," alisisitiza.

Kamanda Muliro pia alisema jeshi hilo linafanya operesheni kusaka wafanyabiashara wanaoficha sukari katika mkoa huo, akisisitiza kuwa muda si mrefu bidhaa hiyo itapatikana kwa wingi.

Pia aliwataka wafanyabiashara waendelee kuuza sukari kwa bei elekezi inayokubalika wakati wakiendelea na operesheni hiyo.




Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu uchunguzi unaoendelea wa mganga wa jadi anayedaiwa kuwanywesha dawa wanafamilia 16 kisha kupoteza fahamu na kuwaibia simu tano na fedha. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mahakama yatoa hati ya kumkamata raia Burundi

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisitu imetoa hati ya kumkamata raia wa Burundi, Marembo Daniel (50) baada ya mshtakiwa huyo kushindwa kufika mahakama huko bila kutoa taarifa yoyote.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya wa Mahakama hiyo baada ya mshtakiwa huyo kushindwa kufika mahakamani huko anakoshtakiwa kuishi nchini bila kibali.

Alisema kwa kuwa mshtakiwa ameshindwa kufika mahakamani, mahakama hiyo inatoa hati ya kumkamata.

Baada ya kutoa maelekezo hayo, Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 20, 2024 kwa ajili ya kusomewa hoja za awali. Upande wa mashtaka ulidai mahakamani huko kuwa umekamilisha upelelezi.

Awali Wakili wa Serikali Raphael Mpuya alidia kesi hiyo iliitwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa hoja za awali baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 11, mwaka jana huko Kurasini, Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam.

Inadaiwa mshtakiwa huyo, akiwa ni raia wa Burundi, alikutwa anaishi nchini bila kibali au viza inayomtambulisha.

# Kipindupindu chaua watatu, wanane wawekwa karantini

**Na Thobias Mwanakatwe, IKUNGI**

WATU watatu wamefariki dunia na wengine wanane wamelazwa hospitalini baada ya kuugua ugonjwa wa kipindupindu ambao umelipuka katika Kata ya Kikio, wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, akizungumza na Nipashe jana, alisema ugonjwa huo ulilipuka katika kata hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita na serikali imechukua hatua haraka kuudhibiti usienee katika kata nyingine.

Alisema kuwa baada ya kutokea ugonjwa huo serikali imechukua hatua kwa kupeleka wataalamu wa afya ambao wanafanya kazi saa 24 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa na karantini imewekwa katika kata hiyo.

Apson alisema uchunguzi wa awali uliofanywa na wataalamu wa afya, umebaini chanzo cha ugonjwa huo ni kutumia maji yasiyo salama, sasa yametengwa maeneo maalum kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa.

"Baada ya kutokea mlipuko huo, serikali mbali na kupeleka wataalamu katika kata hiyo, pia imepeleka vifaa tiba na dawa na nimetoa agizo kwa viongozi wa vijiji vyote wilayani Ikungi kuitisha mikutano ya hadhara kuelimisha wananchi namna ya kujikinga na maambukizi ya kipindupindu," alisema.

Alielekeza wananchi kuchukua tahadhari kwa kuchemsha maji ya kunywa, kunawa mikono vizuri kwa sabuni, kuosha matunda kabla ya kula na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima," alisema.

Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na bakteria aina ya vibrio cholera kwenye utumbo mwembamba, ambaye hutoa sumu inayosababisha kutolewa kwa maji mengi ndani ya utumbo kwa njia ya kuhara na wakati mwingine kutapika na homa kali.

Bakteria hao wanapatikana katika chakula au maji machafu na haja kubwa kutoka kwa mtu aliye na maambukizi.

Kwa ujumla, unaweza kuambukizwa kupitia maji machafu, mboga zilizopandwa kwenye maji taka, samaki na dagaa waliovuliwa kwenye maji machafu, vyakula na vinywaji vilivyo na bakteria hao.

## Hatima kigogo CWT mikononi mwa DPP

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HATIMA ya kesi inayowakabili Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mwalimu Japhet Maganga, na wenzake 10 inasubiri uamuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kama watatakiwa kufikishwa mahakamani au vinginevyo.

Wakili Elias Machibya, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa kuhusu kesi hiyo, alisema wateja wake walipatiwa dhamana juzi kwa sharti na kutakiwa kurudi jana ili wapatiwe maelekezo kuhusu hatima yao.

"Juzi wateja wetu walipatiwa dhamana lakini waliambiwa warudi leo (jana) kuripoti saa 3:00 asubuhi leo (jana). Tumefika muda huo na kuelezwa kuwa tusubiri maelekezo yatakayotolewa na DPP, hivyo turudi tena kesho (leo) kuona kama jalada limeletwa ambalo litaelekeza kama wateja wetu wanafikishwa mahakamani au la," alisema Machibya.

Maganga na wenzake 10 walipata dhamana juzi jioni baada ya kusota mahabusu kwa siku nne kutokana na kushikiliwa na polisi mkoani Dodoma kwa tuhuma za kufanya fujo kwenye mkutano wa Baraza Kuu la CWT wa kupitisha bajeti ya mwaka.

Tukio hili lilitokea Februari 16, 2024 baada ya baraza hilo kuazimia kumsimamisha kazi Maganga kutokana na kupoteza sifa baada ya kufukuzwa kazi na mwajiri wake, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Baada ya baraza hilo kuazimia kwa pamoja kumsimamisha kazi Maganga ndipo zilipozuka fujo, hivyo kusababisha Jeshi la Polisi kuingilia kati na kumkamata yeye na wenzake 10.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, akizungumzia sakata hilo Februari 16, mwaka huu, alisema Maganga na wenzake walikamatwa wakati wa mkutano wa Baraza Kuu la CWT.

"Tulipata taarifa kuwa kuna watu wanafanya fujo tukaenda kudhibiti kabla hayajatokea madhara kwenye mkutano huo sisi hatufahamu ilikuaje zikatokea fujo waulizwe CWT wenyewe," alisema Kamanda Otieno.

# Profesa Janabi: Sitii hofu, sitanii

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema hajawahi kufanya utani; kila anapotoa angalizo kuhusu mlo kwa umma, anafanya hivyo kwa kuzingatia taaluma yake, akisisitiza anaona mstari mwembamba wa uhai kila saa.

Anasema kupitia taaluma yake, anaona ni bora kutoa elimu kuhusu jamii kula mlo usiopindukia ili kulinda afya na hajawahi kumtaka mtu aache kula.

Prof. Janabi aliyasema hayo jana wakati wa mazungumzo maalum na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, akielezea masuala mbalimbali kiafya, hasa jamii kuchukua tahadhari katika mlo na si kuijengea hofu.

"Kuna wakati huwa ninaona watu wanaweka utani, kile ninachokisema wanaambatanisha na picha yangu. Siwezi kuweka utani wakati mimi ni daktari kwa taaluma. Sijawahi kuleta utani. Mimi ninakula mara mbili kwa siku.

"Ninaishi humu (MNH) ndani, ninajua na ninauona mstari mwembamba wa kifo. Ninapotoa ushauri sitanii. Niko humu ndani ninashuhudia mengi na kazi kubwa kwetu ni kuokoa uhai," alisisitiza.

Prof. Janabi alisema kuwa pamoja na teknolojia kubwa kuwapo duniani, kuna magonjwa yanaongezeka hasa yasiyoambukiza, ambayo nchini yanasabisha vifo kwa asilimia 34.

"Hauhitaji fedha tu, unapotoa ushauri kwamba watu wapunguze kula, wangapi wanatii? Kila mmoja ajaribu kwa siku 10 ukishakunywa chai usiguse kitu hadi chakula cha mchana, vilevile hadi usiku usiguse kitu.

"Miaka ya 1970 watu walikuwa wanakula milo mitatu. Mlo ulikuwa kwa utaratibu. Lakini sasa mtu asubuhi mlo, itapita hiki kala, kila kitu mbele yake kikipita anakula, ukihesabu usiku amekula milo mingi.

"Ninakula mara mbili (kwa siku), kwa uzito ninataka nguvu yangu iwe sawa na mwili. Hivyo, itategemeana na mtu na mtu. Unakula kulinda mwili kinga zisishuke sana.

"Nimekunywa chai leo (jana) asubuhi, ni kavu, mchana nimekula na maji, kula tena hadi usiku," alifafanua bingwa huyo wa maradhi ya moyo.

Alisema hoja yake si kwamba watu wale mlo mmoja kwa siku au mitatu, lakini inayozingatia saa na si mlo kila mara bila kuhisi njaa.

"Sijawahi kumkataza mtu kula chakula. Nimesema watu wasile ovyo kwa wastani. Hivi vitu havianzi ghafla, mara moja tunakwenda taratibu. Tujitahidi kupunguza wanga, sukari.

"Sizungumzii sukari hii ya kwenye chai tu. Bali vya kisindikwa, ili viishi muda mrefu vinahitaji kemikali nyingi. Unaponunua angalia maelezo kuna wanga, sukari kiasi gani. Angalia soda kuna sukari kiasi gani.

"Wengi mnasema magonjwa haya ni ya wazee, uko sahihi na hauko sahihi. Wewe leo una miaka 27 au 30 lakini baada ya miaka 15 au 20 utakuwa na miaka 50. Utaanza vidonge na sindano za kisukari," alionya.

Alishauri Watanzania kuwekeza katika afya badala ya kujikita katika kutunza fedha ili ziwe msaada uzeeni. Alisema ni vyema kutunza afya ili iwe msaada uzeeni na kuepuka gharama za matibabu.

"Maana utatunza fedha utakuja kulipia dialysis baadaye au matibabu ya moyo. Wengi 'wanasema pombe kama haitanui chupa, itatanuaje moyo?' Nimeona wagonjwa wa moyo kwa miaka mingi, mapafu na moyo vinatanuka au kuathiriwa," Prof. Janabi alionya.

Bingwa huyo wa maradhi ya moyo amekuwa anaibua mijadala katika mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kutokana na angalizo analotoa kwa wananchi kuhusu ulaji na matumizi ya vileo.




Diwani wa Kata ya Kisukuru, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Lucy Lugome akifurahi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Magoza, baada ya kukabidhi madawati 200 yaliyotolewa na Mkurugenzi wa Jiji hilo, jana. **PICHA: MHIDINI MSAMBA**

# Bil. 988/- kuleta lami Km 250, masoko 18 na stendi tisa Dar

**Na Faustine Feliciane**

SHILINGI bilioni 988 zinatarajia kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 250, masoko ya kisasa 18 na vituo tisa vya mabasi mkoani Dar es Salaam.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, alisema jana kuwa ujenzi wa miundombinu hiyo ni wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) awamu ya pili ambao pia utaanzisha mfumo wa udhibiti wa taka ngumu.

Mchengerwa alisema hayo baada ya kutia saini mkataba wa fedha za mradi huo kati ya serikali na Benki ya Dunia (WB). Serikali iliwakilishwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba wakati WB ikiwalishwa na Mkurugenzi Mkazi, Nathan Belete.

Waziri Mchengerwa amesema Dar es Salaam imekuwa na changamoto ya miundombinu, ikiwamo ya barabara na kwamba awamu ya kwanza ya DMDP iliboresha kilometa 207 katika halmashauri tatu zilizokuwa chini ya mradi na imeleta mabadiliko makubwa.

"Sasa hivi mradi huu utatekelezwa kwenye halmashauri zote za mkoa wa Dar es Salaam. Kila halmashauri itajengewa barabara za lami, masoko na vituo vya mabasi. Mradi unaenda kuangalia changamoto ya usimamizi wa taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla wake.

"Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya taka kutochukuliwa kwa wakati na vilevile makandarasi wa kukusanya taka ngumu kuwa na mazingira ambayo si rafiki kwa kufanya majukumu yao kwa ufanisi. Mradi huu unatarajiwa kuboresha miundombinu ya taka ngumu kwa maana ya kuanzia katika ukusanyaji, usafirishaji hadi utunzaji wake katika madampo ya kisasa matatu yanayotarajiwa kujengwa chini ya mradi huu," alisema Mchengerwa.

Pia alisema kupitia mradi huo, mifereji mikubwa ya maji ya mvua itaboreshwa na mifereji muhimu itatambuliwa na itajengwa yenye jumla ya kilometa 90 kwa Dar es Salaam nzima.

"Mradi huu ni ishara kuwa serikali ina nia thabiti ya kutatua changamoto za miundombinu ya Dar es Salaam na kubadilisha hali ya Jiji letu," alisisitiza Mchengerwa. Waziri Nchemba alisema mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miaka sita kuanzia mwaka 2024/25 na gharama yake ni EURO milioni 361.1 sawa na Sh. bilioni 988.083 na utaleta mabadiliko chanya makubwa katika Jiji la Dar es Salaam.

Naye Belete alisema ni fahari kwao kushiriki katika kukuza na kuendeleza Jiji la Dar es Salaam na kubainisha kwamba kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita, Benki ya Dunia imetoa zaidi ya Dola bilioni 1.5 kwa ajili ya uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam.

Benki ya Dunia kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI wamekwishatoa fedha nyingi kwa ajili ya kutatua changamoto za miji ya Tanzania hasa katika kuboresha miundombinu muhimu ya mijini ikiwamo mradi wa ULGSP, TSCP pamoja na DMDP awamu ya kwanza na kwa sasa wametoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa TACTIC katika miji 45 nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada zifanyike kukomesha tatizo la mikopo kausha damu

**KWA** miaka kadhaa sasa, kumekuwa na vilio kutoka kwa makundi ya watu mbalimbali kuhusu mikopo ambayo badala ya kuleta ahueni ya maisha kwao, imegeuka kuwa maumivu na hata kusababisha wengine kupata maradhi kama vile kiharusi, msongo wa mawazo, kisukari na shinikizo la damu na baadhi kufariki dunia.

Mikopo hiyo ambayo kutokana na kusababisha maumivu hayo, imebatizwa majina mbalimbali yakiwamo 'mikopo umiza' na kaisha damu. Mtu anaweza kukopa kiasi kidogo cha fedha lakini riba pamoja na mkopo anajikuta akilipa asilimia 200 au zaidi. Makundi ambayo yameumizwa kwa kiasi kikubwa ni watumishi wa umma hasa walimu na kinamama ambao hujishughulisha na biashara ndogo ndogo.

Licha ya kulipa riba kubwa, baadhi ya watu waliotumbukia katika mkumbo huo wamejikuta wakipoteza mali kama vile samani za ndani, magari, mashamba na hata nyumba zao kupigwa mnada. Matokeo ya yote hayo ni watu kurudi kwenye umaskini na wengine kupoteza maisha kutokana na kukumbwa na maradhi yasiyo ya kuambukiza.

Mikopo hiyo, kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inatolewa kwa njia zisizo rasmi kwa maana ya vikundi ambavyo havijasajiliwa kisheria na watu binafsi ambao wamekuwa wakishawishi wananchi kukopa kwa kuwapa kauli tamu lakini baadaye kugeuka kuwa machungu kwao, hivyo kusadifu kwa msemo maarufu wa kukopa harusi kulipa matanga.

Kwa ujumla, mikopo hiyo imetokana na kuwapo kwa wimbi la wakopeshaji mtandaoni ambao masharti ya ukopaji yamegubikwa na usiri na BoT inatafsiri mtindo huo mpya wa ukopeshaji umehamia zaidi mtandaoni. Wajanja hao wanatumia faida ya kuwapo mitandao na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano kujinufaisha huku wakiacha maumivu kwa watu wengine.

Jambo la kushangaza ni kwamba kwa muda mrefu, BoT imekuwa ikisisitiza kuwa watu wasirubuniwe na watu hao ambao wamesababisha maumivu kwao badala yake wafuate taratibu kwa kukopa katika taasisi zilizosajiliwa. Pamoja na msisitizo huo, watu wamekuwa na masikio mazito ambayo katu hayasikii dawa.

Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha imeweka masharti kila anayekopesha fedha, afuate taratibu na kwamba atakayekwenda kinyume, adhabu ni faini ya Sh. milioni 10 au kifungo gerezani au vyote kwa pamoja. Licha ya kuwapo msisitizo huo na kuwapo kwa sheria, swali la kujiuliza ni kwa nini tatizo hilo bado linazidi kuota mizizi?


Suala hili linapaswa kufanyiwa kazi kwa taasisi husika za serikali kuchukua hatua zinazotakiwa katika kulikomesha ili lisiendelee kuwaumiza wananchi. Baadhi ya vikundi au watu wanaojihusisha na biashara hiyo wanajulikana, hivyo vyombo vya dola havina budi kufanya kazi yake katika kupunguza athari zinazoendelea katika jamii kutokana na mikopo hiyo iliyojipatia majina kemkemu.

BoT kwa kushirikiana na taasisi zingine za fedha hususan benki, inapaswa kuongeza kutoa elimu kwa umma kuhusu suala hili hasa kwa watu walioko maeneo ya pembezoni ambao kwa sasa ndio waathirika wakubwa. Elimu hiyo haina budi kuwa shirikishi kwa maana ya kuhusisha wadau wengine kama vile vyombo vya habari, wanasiasa na viongozi wa dini.

Pamoja na njia hiyo ya kutoa elimu, ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kutoa mwongozo wa kupunguza masharti ya utoaji mikopo kwa taasisi za fedha ikiwamo kiwango cha riba ili kuwezesha wananchi wengi kupata huduma hizo na kuondokana na adha ya kujiingiza katika mikopo umiza.

Ni wazi kwamba wimbi la watu kukimbilia katika mikopo hiyo, maarufu kama kausha damu au mikopo umiza ni matokeo ya kutokuwapo kwa fursa wezesha kwa wananchi kupata mikopo yenye masharti nafuu. Kwa maneno mengine, kuna ulazima wa kuangalia na kubaini ombwe linalosababisha watu kuumizwa na kausha damu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Wapigakura wanasubiri mgawanyo majimbo

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kutangaza utaratibu na sifa za kugawa majimbo mbalimbali, ikiwa ni sehemu ya maandalizi kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka ujao.

Hayo ni maelezo ya Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Ummy Nderiananga bungeni hivi karibuni, wakati akijibu swali la mbunge wa Nachingwea, mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile aliyetaka kufahamu ni lini serikali itagawa jimbo hilo.

Katika ufafanuzi wake ni kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeipa tume hiyo mamlaka ya kuchunguza mara kwa mara maeneo ili kugawa mipaka ya majimbo ya uchaguzi angalau kila baada ya miaka 10 baada ya kupata kibali kutoka kwa Rais.

Ni kweli kwamba yapo baadhi ya majimbo ambayo ni makubwa, na wakati mwingine ukubwa huo unaweza kusababisha wananchi kutofikiwa na huduma za kijamii zikiwamo za afya, elimu na nyingine muhimu.

Nachingwea ni miongoni mwa majimbo makubwa ambalo lina kata 36 ambazo ninaamini kuwa kuzifikia, wakati mwingine inaweza kuwa vigumu, hivyo kuzipunguza na kuanzisha jimbo lingine ninadhani ni jambo la muhimu.

Hata mbunge huyo mwenyewe wa Nachingwea anaeleza kuwa linapotoka fungu la fedha, kwa ajili ya maendeleo ya jimbo halizingatii idadi ya kata, kitendo ambacho anakifafanua kuwa ni kukwamisha maendeleo.

Kwa mazingira hayo, ninadhani ni vyema majimbo makubwa kama hilo la Nachingwea yakagawanywa ili kuharakisha maendeleo, kwani baadhi ya mikoa kuna majimbo yana kata chache kama 14.

Ninatambua kuwa idadi ya watu katika eneo linalokusudiwa kugawanywa ni kigezo muhimu, kwani ndio msingi wa demokrasia ya uwakilishi, lakini pia idadi ya watu inatakiwa kuwa sawa kwa kila jimbo.

Wakati mwingine kunaweza kuwa na ugumu wa kuwa na idadi ya watu inayofanana katika majimbo yote, lakini ninaamini ukubwa wa jimbo ni wazi unaweza kuwa kikwazo cha wananchi kufikiwa na maendeleo.

> **Kwa mazingira hayo, ninadhani ni vyema majimbo makubwa kama hilo la Nachingwea yakagawanywa ili kuharakisha maendeleo, kwani baadhi ya mikoa kuna majimbo yana kata chache kama 14.**

Ugawaji wa majimbo makubwa unaweza kusaidia upatikanaji wa njia za mawasiliano, kumrahisishia mwakilishi wa wananchi kuwafikia au kuwasiliana nao kirahisi na kuchukua hoja zao kuzipeleka bungeni.

Labda nikumbushe kuwa wakati tume ikiwa katika mchakato wa kutaka kugawa majimbo, ninaamini mipaka ya kiutawala itazingatiwa, ili hata kama itabadilika basi kusiwe na malalamiko.

Mara kadhaa kumekuwapo na malalamiko wakati wa kugawanya mitaa, kata na hata majimbo, huku baadhi ya wananchi wakikataa kubaki au kuhamia eneo jipya wakidai ugawanyaji wa mipaka umekosewa.

Hivyo, wakati huu ambao tume inajiandaa kufanya kazi ya kugawa majimbo, kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ingejipanga kuhakikisha kwamba malalamiko ya aina hiyo hayajirudii, ili kuharakisha maendeleo ya majimbo.

Kimsingi, tume ina utaratibu wa kuchunguza mipaka na kugawa majimbo ya uchaguzi kufanya mikutano na wadau kwa kujadili vigezo na utaratibu unaotumika katika kuchunguza mipaka na kugawa majimbo.

Vile vile, huwa inatangaza kwa wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kuhusu nia ya kufanya zoezi la kuchunguza mipaka na kugawa majimbo, katika matangazo hayo vigezo na utaratibu unaotumika huwa vinawekwa wazi.

Kwa mantiki hiyo, ingekuwa ni vyema wananchi kuchangamkia fursa ya kuhudhuria mikutano ya tume ili kujadili vigezo na utaratibu unaotumika katika kuchunguza mipaka na kugawa majimbo.

Iwapo watahusika katika hatua hizo kuanzia mwanzo hadi mwisho, ninaamini hakutakuwa na malalamiko kama ambayo yamewahi kutokea miaka ya nyuma wakati wa kugawa majimbo ya uchaguzi.

Ikumbukwe kuwa lengo la serikali na wadau wake ni moja la kuwaletea wananchi maendeleo, hivyo kufanikisha mpango huo wa tume ni kuharakisha maendeleo ya wananchi na ya maeneo husika.

# TANAPA yaona fursa Siku ya Wanawake

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) linatarajia kupeleka wanawake kufanya utalii katika Hifadhi ya Taifa Nyerere.

Mpango huo una lengo la kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha utalii na uhifadhi nchini.

Mkoani Dar es Salaama juzi, Kamanda wa Uhifandi Kanda ya Kusini, Steria Ndaga, akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa TANAPA, alisema katika kuadhimisha siku hiyo (huadhimishwa Machi 8 kila mwaka) mwaka huu, wataanza kwa hafla maalum Machi 2, mwaka huu jijini Dar es Salaam na kumalizikia Hifadhi ya Taifa Nyerere.

Alisema lengo la hafla hiyo ni kupeleka wanawake kuona vivutio mbalimbali vilivyoko katika hifadhi hiyo iliyoanzishwa na Rais John Magufuli baada ya kumegwa Pori la Akiba Selous.

Pia wana dhamira ya kuhamasisha uhifadhi na umuhimu wake, wakishirikiana na uongozi wa Reli ya Tanzania - Zambia (TAZARA).

"Lengo la safari hii ni kuhamasisha watanzania kuona umuhimu na fursa mbalimbali zilizoko katika hifadhi za taifa.

"Wanawake kwa umoja wetu tuko wengi kuliko wanaume, hivyo tukitumia hii fursa vizuri tutaendeleza hizi jitihada za Rais Samia ambaye amehakikisha kuwa uhifadhi wa mazingira unaendelea nchini.

"Pia kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour, tunaweza kuongeza kipato cha watanzania kwa kupokea watalii wengi ambao kimsingi wameshaanza kuonekana wakija kutoka kona mbalimbali za dunia. Hivyo, tukiunga mkono kwa pamoja shughuli hizi za uhifadhi, tutaongeza uchumi wetu wa nchi," alisema Ndaga.

Alibainisha kuwa katika safari hiyo ya Machi 2, mwaka huu, kila mtu atagharamia Sh. 200,000 ambayo itamwezesha kutoka Dar es Salaam hadi Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa usafiri wa treni, akiona vivutio mbalimbali vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo.

Kamanda Steria alibainisha kuwa Ukanda wa Kusini mwa Tanzania haujahamasika kwa kiasi kikubwa katika shughuli za utalii, akitoa rai kwa wananchi kutembelea hifadhi hizo zikiwamo za Nyerere, Saadani, Mikumi, Ruaha, Katavi na Kitulo ili kuendeleza na kuongeza tija ya uhifadhi nchini.

Vilevile, alieleza kuwa katika safari hiyo, malengo yao ni kupata wanawake zaidi ya 400 kwa kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere iko karibu na miji mikubwa ya Dar es Salaam na Morogoro na ni rahisi kufikika kwa usafiri wa gari, treni na ndege.

Judita Ligenzi, mmoja wa madereva wa treni za TAZARA atakayeongoza garimoshi siku ya safari hiyo, alihimiza wanawake kutumia fursa hiyo kuongeza tija yao katika kuendelea kuhamasisha utalii nchini.

"Tutahakikisha kwamba safari hiyo itakuwa salama wakati wa kwenda na kurudi, pia hifadhi hii inafikika kirahisi, hivyo tunaomba wanawake mje ili wawe wajumbe wazuri kwa wengine," alisema Ligenzi.

Hifadhi ya Taifa Nyerere ndiyo hifadhi kubwa zaidi nchini. Ianzishwa mwaka 2019 ikiwa na eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 54,600. Imezingirwa na mikoa ya Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Eneo hilo ni kubwa kushinda nchi 70 duniani ikikadiriwa kuwa na eneo sawa na nchi ya Costa Rica (Amerika ya Kati) na takribani mara mbili ya ukubwa wa nchi ya Ubelgiji (Ulaya).




Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara Chama cha ACT- Wazalendo, Halima Nabalang'anya, akionyesha fomu ya kuwania nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho Kanda ya Kusini, baada ya kuichukua makao makuu ya ACT, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Sheria mpya Shule ya Sheria yaja na mabadiliko mengi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni mapendekezo ya kufanyiwa marekebisho Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 ili kuondoa vikwazo mbalimbali vilivyobainika katika utekelezaji masharti ya sheria.

Muswada wa marekebisho hayo ulisomwa kwa mara ya kwanza bungeni katika Mkutano wa 14 wa Bunge uliomalizika wiki iliyopita.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alielekeza muswada huo kushughulikiwa na Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Joseph Mhagama, akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa kamati kwa mwaka 2023, alisema serikali itapeleka marekebisho ya sheria hiyo bungeni ili kuboresha masuala ya mafunzo ya sheria kwa vitendo na ufaulu wa wanafunzi.

Kufanyika marekebisho hayo kunatokana na mapendekezo ya Kamati ya Dk. Harrison Mwakyembe iliyokuwa inatafuta chanzo cha kufeli idadi kubwa ya wanafunzi waliofanya mitihani ya mafunzo ya uanasheria kwa vitendo katika shule hiyo. Kamati hiyo iliundwa mwaka juzi na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro.

Pamoja na mambo mengine, Kamati ya Mwakyembe ilishauri serikali iunde Sekretarieti ya Baraza la Elimu ya Sheria (CLE) na kuipa bajeti na ofisi yake ili kutekeleza majukumu yake ya kusimamia taaluma zote za sheria nchini.

**MUSWADA UNA NINI?**

Inapendekezwa katika kifungu cha 5 cha muswada huo kurekebishwa kwa kupanua wigo wa majukumu ya Shule ya Sheria ili kujumuisha jukumu la kutoa mafunzo mengine mahsusi katika sekta ya sheria.

Kifungu cha 8 kinapendekeza kurekebishwa kwa kuondoa matakwa ya majukumu ya wakurugenzi kuainishwa katika kanuni na badala yake kuainishwa katika skimu ya utumishi ili kuhakikisha sheria inarejea nyaraka sahihi inayoainisha majukumu ya wakurugenzi.

Kifungu cha 9(2) kinapendekeza kurekebishwa kwa kumwondoa Mkuu wa Taasisi kuwa Katibu wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani na badala yake kumweka Naibu Mkuu wa Taasisi anayehusika na mafunzo ili kuimarisha utekelezaji majukumu ya Kamati kwa kuwa Naibu Mkuu wa Taasisi anayehusika na mafunzo ndiye mwenye jukumu mahsusi la kusimamia masuala ya mafunzo na mitihani katika Shule ya Sheria.

Kifungu cha 9(4) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha muda wa ujumbe wa wajumbe wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani ili kuhakikisha kuwa muda wa wajumbe kutoa huduma unatamkwa bayana katika sheria.

Kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua katika sheria nafasi ya Naibu Mkuu wa Taasisi Anayehusika na Mafunzo na Naibu Mkuu wa Shule ya Sheria Anayehusika na Utawala ili kutambua nafasi hizo muhimu katika uongozi wa shule hiyo ambazo kwa sasa hazijatambuliwa katika sheria.

Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubadili muundo wa Bodi ya Shule ya Sheria ili kujumuisha wajumbe ambao si wanasheria.

Vilevile, kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hicho kinarekebishwa ili kuainisha mamlaka ya uteuzi ya wajumbe wa bodi ambao hawaingii kwa nafasi zao za madaraka.

Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha kuwa wajumbe wa bodi watalipwa ada kadri itakavyoamuliwa na Msajili wa Hazina ili kutambua nafasi ya Msajili wa Hazina katika kuamua ada na stahili za wajumbe wa bodi.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# Tanzania, Misri kushirikiana kibiashara sekta ya uchukuzi

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imetangaza kuendeleza ushirikiano wa kibiashara na Misri katika sekta ya uchukuzi ili kuleta maendeleo na kukuza uchumi wa nchi.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kuweka mikakati ya kukuza ushirikiano baina ya Tanzania na Misri kwenye sekta ya uchukuzi.

Alisema ushirikiano wa diplomasia baina ya mataifa hayo ni wa muda mrefu, hivyo kikao kilichofanyika ni kikubwa na kina dhamira ya dhati kuendeleza ushirikiano wa kibiashara baina ya mataifa hayo mawili.

Alisema kazi kubwa iliyofanywa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa fedha nyingi za kuboresha miundombonu, imeleta mafanikio hususani sekta ya usafirishaji.

Prof. Mbarawa alisema wamekutana na Waziri wa Uchukuzi wa Misri aliyeambatana na wawekezaji wakubwa, wataalamu mbalimbali kuwapa uzoefu na kutazama fursa zilizopo hususan katika sekta hiyo.

"Tanzania tuna fursa tele, tunawakaribisha katika sekta ya bandari hususan ujenzi wa gati 13, 14 na 15 katika Bandari ya Dar es Salaam. Serikali inawakaribisha kufanya uwekezaji katika eneo hili kwa sababu tunashirikisha sekta binafsi na maeneo ikiwamo anga," alisitiza Prof. Mbarawa.

Waziri wa Uchukuzi wa Misri, Luteni Jenerali Kamel Alwazeer, alisema wamekuwa na ushirikiano mzuri na Tanzania toka enzi za Rais Gamal Abdel Nasserna na Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema Tanzania ni kitovu cha usafiri na usafirishaji ndani ya Afrika Mashariki kutokana na kuwapo Bandari ya Dar es Salaam ambayo imekuwa na ufanisi mkubwa kwa nchi.

"Kupitia mkutano huu tutaanza ushirikiano baina ya Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Savaga iliyoko kwetu Misri kubadilishana uzoefu na utalaamu," alisema.

Kuhusu mkutano huo, alisema ni muhimu na una lengo la kuendeleza ushirikiano uliopo kwa mataifa hayo ambayo yamekuwa yanashirikiana kwa muda mrefu.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Kisena Mabuba (mwenye kofia), akikabidhi msaada wa kiti mwendo kwa mwanafunzi Emmanuel Dotto wa Shule ya Msingi Iselamagazi, wilayani humo, kilichotolewa na Shirika la Tanzania Cheshire Fundation juzi, kwa ajili ya usafiri wa kutoka nyumbani kwenda shule ili apate haki yake ya kupata elimu katika mazingira rafiki na kutimiza ndoto zake. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TPSF yapata dawa pengo la ujuzi kwa wahitimu

**Na Mwandishi Wetu**

MWONGOZO wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) katika kutoa mafunzo tarajali na kuwekeza kwa vijana, umeigusa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Mkurugenzi wa TPSF, Raphael Maganga ametoa rai kwa kampuni za sekta binafsi kuiga mwongozo wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) katika kutoa mafunzo tarajali na kuwekeza kwa vijana wa kitanzania katika mustakabali wa Tanzania.

Pia amesema kuna haja wadau wa TPSF kuendelea kudumisha ushirikiano kati ya wafanyabiashara na wawekezaji na taasisi za elimu ni muhimu katika kuziba pengo la ujuzi wa madini barani Afrika.

Maganga alieleza hayo mwishoni mwa wiki mjini Geita wakati wa hafla ya kukaribisha wahitimu 40 wa vyuo mbalimbali wasio na ajira ambao wamepatiwa fursa ndani ya GGML kupata mafunzo ya vitendo kazini kwa muda wa mwaka mmoja sambamba na wahitimu 10 wa mafunzo hayo kwa mwaka jana ambao wamepata ajira ya kudumu ndani ya kampuni hiyo.

Mbali na kupongeza GGML kwa mpango wa mafunzo kazini kwa vitendo, Maganga pia alisema mpango huo si tu unatoa fursa pekee, bali pia unaziba pengo la ujuzi nchini na kuwawezesha vijana wa kitanzania kwa ajili ya kesho iliyo bora zaidi.

"Kwa kutoa mafunzo ya kazi na fursa nyinginezo, tunaweza kuziba pengo kati ya elimu na ajira na kuhakikisha kwamba vijana wetu wanawezeshwa na ujuzi wanaohitaji ili kufaulu," alisema.

Alisema kuongezeka kwa uchimbaji madini barani Afrika kumesababisha uhitaji mkubwa wa ujuzi ambao ni adimu barani na si suala la Tanzania tu, bali la kimataifa.

"Uhaba huu wa vipaji unaonekana hasa katika nchi kama Angola, Nigeria, Tanzania na Ghana. Ili kukabiliana na hili, kuna haja ya kuboresha programu za mafunzo, huku kampuni za sekta binafsi zikichukua jukumu muhimu katika kufadhili na kuunda mitaala ili kukidhi mahitaji ya sekta," alisema.

Aliongeza: "Nimefarijika kusikia GGML kwa muda mrefu imekuwa mwanzilishi katika kuunga mkono mipango ya serikali inayolenga kuimarisha uwezo wa wahitimu kuajiriwa nchini.

"Kupitia mafunzo ya kazi na programu nyingine za wahitimu, GGML imekuwa muhimu katika kusaidia wahitimu wapya kupata ujuzi na uzoefu unaohitajika ili kustawi katika soko la ajira. GGML inatupa fahari sekta binafsi nchi hii. Tunajivunia kuwa nayo."

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu Rais Mwandamizi - Kitengo cha Biashara Afrika kutoka AngloGold Ashanti - GGML, Terry Strong alisema tangu kuanzishwa mpango wa mafunzo hayo mwaka 2009, jumla ya wahitimu 218 wa kitanzania wamenufaika.

"Wahitimu hawa si tu wamepata uzoefu muhimu wa kazi, bali pia wamechangia pakubwa katika mafanikio ya GGML. Ni ushahidi wa uwezo wa vipaji vilivyomo ndani ya vijana hawa wa kitanzania," alisema.

# Mabadiliko hali ya hewa yakwamisha marejesho mikopo ya halmashauri

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

BAADHI ya wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na kilimo katika Kata ya Panzuo, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga walionufaika na mikopo ya halmashauri, wanashindwa kurejesha kwa wakati kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Panzuo, Mkanda Muganyi alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya mafunzo ya ujasiriamali kwa Jukwaa la Wanawake wa kata hiyo.

Muganyi alisema wajasiriamali wengi ambao wanajihusisha na kilimo wanategemea zaidi mvua, hivyo isiponyesha, mavuno yanakuwa hafifu na kuchangia kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati.

Aliomba serikali kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji ili wakulima walime kipindi chote na kupata mavuno yatakayowawezesha kuinuka kiuchumi na wanapokopa, warejeshe mikopo kwa wakati.

Katika mafunzo hayo ambayo yamefadhiliwa na Diwani wa Panzuo, Dude Hamis, Ofisa Maendeleo ya Jamii huyo alitaja sababu nyingine ya kusuasua marejesho kwa wanaokopa ni kutumia fedha kinyume cha malengo, pia kukosa elimu.

"Hapa wamepatiwa elimu ya kilimo, ufugaji na ujasiriamali wakitoka hapa watakuwa na mabadiliko kwa wanaochukua mikopo kuendesha shughuli zao," alisema.

Awali wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Diwani Hamis alisema amelazimika kuwezesha mafunzo hayo Ili kuleta mabadiliko kwenye shughuli za ujasiriamali na ufugaji.

Alisema mafunzo hayo yatakuwa yanafanyika kila baada ya miezi mitatu kwa vikundi tofauti na wanaonufaika watafikisha elimu hiyo ngazi ya kijiji na vitongoji ili kuleta mabadiliko kwenye nyanja zote.

Zakia Msangi, mmoja wa washiriki, alishukuru diwani huyo kwa kufadhili mafunzo hayo, akiamini watainuka kwa kuwa wamepata elimu ya ufugaji, kilimo na ujasiriamali.

Wengi wa wajasiriamali wanaonufaika na mikopo ya halmashauri katika kata hiyo, wanajishughulisha na kilimo na ufugaji.



# Serikali yatafuta suluhu wanaohujumu maliasili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewaita mezani waendesha mashtaka na wapelelezi wa Jeshi la Polisi nchini na kuzungumza nao kuhusu mustakabali wa watu wanaohujumu wanyamapori, misitu na viumbe wa baharini.

Wadau hao wa haki jinai, walikutana jana jijini hapa na Waziri wa Katiba na Sheria Dk. Pindi Chana, ambaye pamoja na mambo mengine, alizindua miongozo miwili ya uendeshaji wa mashtaka ya wanyamapori, misitu na uvuvi ili kudhibiti ujangili na uvuvi haramu.

Katika kikao kazi hicho, Waziri Chana, alisema miongozo hiyo itawasaidia wadau wa kesi hizo, kuziendesha kwa haki na kuleta manufaa kwa rasilimali nchini.

"Jukumu la kulinda rasilimali zetu ni sisi wenyewe, hivyo ninaamini wapelelezi na waendesha mashitaka kwa sasa mtasaidia kukomesha ujangili wa wanyamapori, uvuvi haramu kwenye maziwa na bahari, lakini pia kukomesha uharibifu wa misitu yetu,"alisema.

Waziri Chana alisema rasilimali zilizopo nchini zinachangia Pato la Taifa na fedha hizo zinafanikisha kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kiongozi huyo aliwatahadharisha wanaojihusisha na ujangili wa rasilimali za taifa kuacha, kwa kuwa wadau wa maeneo hayo wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakomesha tabia hizo.

Waziri Chana alisema taifa haliwezi kuacha baadhi ya watu wakiendelea kuvuna rasilimali za nchi kwa manufaa yao peke yao bila kufuata sheria, hivyo ni lazima wadhibitiwe.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), Sylvester Mwakitalu, alisema uzinduzi wa miongozo hiyo utasaidia kupunguza uhalifu wa rasilimali nchini.

"Tumeona tuhuishe Mwongozo wa Usimamizi wa Wanyamapori na Misitu na Mwongozo wa Mazao ya Uvuvi.

"Sababu tumeona tusipokuwa makini katika kulinda rasilimali zetu kama bahari na maziwa yatabaki tupu kutokana na uvunaji haramu wa mazao haya unavyozidi kushamiri,"alisema.

Mwakitalu alisema kuna wakati makosa hayo yanafanywa kwa kupanga na baadhi wanaotoka nje ya nchi, hivyo kupitia miongozo hiyo itawasaidia kudhibiti uhalifu huo. Alisema katika ukusanyaji wa ushahidi wa makosa hayo kupitia miongozo hiyo, itasaidia kufanywa kisayansi, teknolojia na kielektroniki na mafunzo hayo yatatolewa nchi nzima kwa wadau wa sekta hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini, Javelin Rugaihuruza, alisema Ofisi ya DPP imeona kuna umuhimu wa kuandaa mafunzo hayo ili kufundisha wadau mbinu mpya zinazotumiwa na wahalifu wa rasilimali za nchi kwa manufaa ya taifa.

Kwa upande wake, Katto Wambura, kutoka Umoja wa Mataifa Ofisi ya Madawa na Uhalifu (UNODC), alisema watatengeneza APP itakayowezesha kuisoma miongozo hiyo kwenye simu pamoja na kusoma miongozo ya nchi nyingine.

## Wanaotumia mkojo wa binadamu, chumvi kutibu red eyes hatarini

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

DAKTARI Bingwa wa Macho wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), Hussein Tayebji, amehadharisha wanaotumia mkojo wa binadamu na maji ya chumvi kuweka kwenye macho kama tiba ya ugonjwa wa red eyes.

Mtaalam huyo amesisitiza kuwa, wanaofanya hivyo kama tiba wanaweza kupata upofu. Tahadhari hii imetolewa baada ya ugonjwa huu kuenea karibu mikoa yote nchini.

Dk. Tayebji ambaye pia ni, Mratibu wa Macho wa Mkoa wa Tanga, alisema mpaka sasa zaidi ya wagonjwa 90 wameugua ugonjwa huo, huku asilimia kubwa wakitokea Jiji la Tanga.

Ugonjwa huo wa maambukizi kwenye ngozi ya juu ya gololi la jicho, unaoitwa Conjunctivitis, maarufu red eyes umesambaa mikoa 26 nchini.

Kutokana na kasi ya ugonjwa huo, amewasihi wananchi wanapougua ugonjwa huo, kwenda kwenye vituo vya afya au hospitali, kwa ajili ya kuwaona madaktari ili kupatiwa matibabu na kupewa ushauri nini wafanye.

"Watu waache kutumia mitishamba, kuweka mkojo kwenye macho au maji ya chumvi kwa sababu kufanya hivyo, kunaweza kusababisha matatizo makubwa kiafya.

"Hatushauri mtu anapopata ugonjwa huu atumie dawa za mwenzake, ukifanya hivyo, maana yake unatumia dawa vibaya na unaweza kupata matatizo makubwa," alisisitiza.

Ugonjwa huu uliripotiwa mara ya kwanza Januari 13, mwaka huu ambapo athari hasi ni vidonda kwenye kioo cha jicho vinavyoweza kusababisha kovu kwenye jicho litakalomfanya mgonjwa apate uoni hafifu au kupoteza uwezo wa kuona kabisa.




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Japhet Simeo (wa tatu kushoto), akifafanua jambo kwa wanachama wa Kundi la Sema na Tanga, waliofanya ziara ya kutembelea Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo Bombo juzi, ili kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali. Kushoto ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Frank Shega. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

## DC Hai aonya madiwani wasionadi yaliyofanyika

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Amiri Mkalipa, amewapa angalizo madiwani wa wilaya hiyo, waliosahau kurudi kwa wananchi wajipime kwa kuwa, moja ya mambo watakayopimwa nayo ni mikutano ya wananchi pamoja na alama alizoacha.

Aliwakumbusha kuwa kinga yao ya kuendelea kuwa diwani wanapaswa kuwaeleza wananchi kila hatua ya wanachofanya kwa maslahi mapana ya umma, kutatua kero zao au kuzitafutia majibu ngazi nyingine.

Mkalipa alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na madiwani hao, baada ya kupewa nafasi ya kutoa nasaha za serikali katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Wilaya hiyo.

"Tunao uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu. Tumejiandaaje? Madiwani mtusaidie. Nendeni mkafanye mikutano na kuwaeleza wananchi yale mliyoyafanya ya maendeleo.


"Na kero mlizotatua waambieni na zile ambazo ziko hatua nyingine zinashughulikiwa waambieni. Hili ni jambo la maana sana hasa kipindi hiki.

"Waelezeni pia wananchi yale mliyowaahidi mmefikia wapi? Wakati wa kuandaa mikutano ni sasa. Niwakumbushe kwamba, tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. Mnawajibu kama viongozi kuhakikisha mnasitawisha chama kilichowaweka madarakani," alihimiza.

Pia aliwataka wazungumzie Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ili kusaidia kipindi kijacho kuwainua wenyeviti wa mitaa, wenyeviti wa vitongoji na vijiji, kwenye uchaguzi.

Awali, Ofisa Serikali za Mitaa, Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Gasper Ijiko, aliwakata madiwani kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri hiyo, kuhakikisha wanakusanya mapato ili kufikia malengo waliyokusudia.

Kaimu Mkurungenzi wa Halmshauri hiyo, Rajabu Yateri, aliishukuru serikali kwa kuipa Wilaya ya Hai, mahindi ya chakula tani 18 .6 zitakazouzwa kwa wananchi kwa bei nafuu ili kukabiliana na upungufu wa chakula.





# TPDC yapewa siku saba kuwasilisha kampuni zisizolipa ushuru huduma

**Na Shaban Njia,** NZEGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imetoa siku saba kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwasilisha taarifa ya kampuni zote zinazofanya kazi ndani ya mradi wa mafuta ghafi bila kulipa ushuru wa huduma (Service levy) na CSR katika halmashauri.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Deus Sangu, alitoa agizo hilo juzi walipotembelea mradi wa yadi ya mtambo wa kuandaa mabomba yatakayotumika kusafirishia mafuta ghafi, uliojengwa katika Kijiji cha Sojo Kata ya Igusule Halmashauri ya Nzega, mkoani Tabora.

Alitoa agizo hilo baada ya wajumbe wa kamati hiyo kuhoji ni namna gani Halmashauri ya Nzega inanufaika na huduma ya ushuru wa huduma na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR) kulingana na uwapo wa kampuni zinayofanyakazi ndani ya Mradi wa Boma la Mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

"Tunaomba kupata taarifa hiyo ili tufahamu kampuni zinazolipa na zile zisizolipa na kwa nini hazifanyi hivyo ili hatua stahiki zichukuliwe na kuziongezea mapato halmashauri," aliongeza Sangu.

Kamishna wa Mafuta kutoka Wizara ya Nishati, Fakhi Mohamed, aliahidi kutekeleza agizo hilo kwa muda uliotolewa ikiwa ni pamoja na kampuni zilizomaliza mikataba yake ili kuhakikisha zile ambazo hazikulipa zinabanwa na kulipa fedha hizo.

Mratibu wa Mradi wa ECOP Taifa, Kisamarwa Joseph, alisema mradi huo ulianza Februari, 2021, na unatarajia kukamilika Desemba, 2025.

Alisema jumla ya wananchi 9822 kati ya 9898 waliopitiwa na mradi huo nchini nzima wameshalipwa fidia zao zaidi ya Sh. bilioni 34.9.

Alisema wananchi 76 wanaendelea kusubiri kwa sababu ya kuibuka kwa migogoro ya kifamilia hususani ya mirathi na kesi zao zitakapokwisha watalipwa fedha zao, kwani zipo kwenye akaunti maalumu.

Alisema kati ya mambo muhimu yaliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbadala 339 kwa ajili ya kaya 344 zilizopoteza ambapo nyumba 12 zilijengwa katika Kijiji cha Sojo na makandarasi wazawa kwa kutumia vifaa na vibarua wa kutoka katika jamii.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (kushoto), akipokea zawadi ya ukumbusho kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc), Takashi Araki, baada ya kufungua warsha kuhusu biashara haramu ya sigara, iliyoandaliwa na TCC, mjini Kigoma juzi, na kuwakutanisha wadau mbalimbali kujadili changamoto za ukuaji wa biashara hiyo katika mikoa ya mipakani na athari yake kwenye mnyororo wa thamani wa usambazaji wa tumbaku na uchumi kwa ujumla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakwamisha miradi kwa kutunishiana misuli

**Daniel Limbe,** CHATO

MIRADI ya maendeleo wilayani Chato imetajwa kutekelezwa chini ya kiwango kutokana na baadhi ya watumishi wa idara mbalimbali kutunishiana misuli.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, mkoani Geita, Mhandisi Deusdedith Katwale, aliyasema hayo juzi wakati akiongea na watumishi.

"Unakuta Mhandisi anakwenda kivyake, ofisa manunuzi kivyake na wakuu wa idara zinazotekeleza miradi husika nao kivyao, kwa staili hiyo hatuwezi kufika hata kidogo badala yake mnapaswa kushirikiana, kusaidiana na kukosoana kwa staha," alisema Katwale.

Alisema inasikitisha kuona miradi inatekelezwa chini ya kiwango kutokana na baadhi ya wakuu wa idara kutoelewana huku akiwasihi kufanya kazi kwa uwazi, ukweli na uzalendo kwa manufaa mapana ya jamii badala ya kulenga kutaka kujinufaisha kwa maslahi binafsi.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Wilaya alitoa siku 90 kwa maofisa afya kata, watendaji kata pamoja na vijiji na maofisa tarafa kusimamia utekelezaji wa usafi wa mazingira, kwa kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo bora na kusisitiza kuwa, agizo hilo ni amri wala siyo hiari.

"Atakayekaidi sheria ichukue mkondo wake, haiwezekani kwa karne hii watu kuendelea kuhimizwa kujenga vyoo, ni muhimu kuzingatia afya ya jamii ili kuepuka magonjwa mbalimbali," alisema Katwale.

Ofisa Afya Wilaya hiyo, Fransisca Charles, amekiri kuwapo kwa baadhi ya kaya ambazo hazina vyoo na kwamba, mkakati umewekwa kuhakikisha kaya zote zinafikiwa na kuelimishwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa matangi ya maji kwenye baadhi ya shule za msingi.

Alisema wilaya hiyo inakabiliwa na uhaba mkubwa wa maofisa afya kata na kwamba, waliopo ni saba kati ya 23 wanaotakiwa.

# Matokeo ya sensa ya watu kutumika kupanga bajeti

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Wiliamu Jijimya, amesema halmashauri hiyo itaanza kutumia matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 katika upangaji wa bajeti ili kuleta usawa wa kimaendeleo kwa kila kata.

Alitoa kauli hiyo juzi katika Mafunzo ya Usambazaji na Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, yalitolewa wilayani humo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu NBS kwa viongozi mbalimbali na makundi ya kijamii.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliwasisitiza viongozi mbalimbali wilayani humo wakiwamo madiwani kwamba, katika upangaji wa mipango yao ya maendeleo, wahakikishe wanatumia matokeo hayo kuleta usawa. Alisema matokeo ya sensa ndiyo msingi wa kufanya uamuzi wa maendeleo kwa kuangalia idadi ya watu kwa kila eneo na uhitaji wa kitu fulani na hatimaye kuleta usawa wa kimaendeleo na kutatua changamoto zinazokabili wananchi.

Alisema matokeo hayo yanabainisha hali halisi ya upatikanaji wa ubora wa huduma za kijamii kama vile maji, miundombinu ya barabara, afya, elimu, nishati, masoko, hivyo takwimu za sensa ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu na kuchochea kasi ya maendeleo na kutatua kero za wananchi.

"Zaidi tuzingatie mwenendo wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuleta usawa," alisema Mkude.

Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Benedict Mugambi, ambaye ni Meneja Idara ya Shughuli za Kitakwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa viongozi na makundi mbalimbali ya kijamii kuhusu matumizi ya matokeo ya sensa katika uandaaji na utekelezaji wa programu za maendeleo.

Mtakwimu Mwinyi Omary kutoka NBS akiwasilisha taarifa za usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022, alisema Tanzania kwa sasa ina idadi ya watu milioni 61.7.

Alisema kwa Mkoa wa Shinyanga wapo watu milioni 2.2 na Wilaya ya Shinyanga ni 468,661, Kahama Manispaa 453,654, Ushetu 390,593, Msalala 378,214, Kishapu 335,483 na Manispaa Shinyanga 214,744.

Ukurasa 13



**UNAPOGONGA HODI UCHAGUZI... MWENYEKITI CCM TANGA ATUMIA MTAJI WA RAIS, MAKONDA KUWASHA MOTO UWAJIBIKAJI**

Ukurasa 14





**Ndivyo moto wa 50/50 unavyowaka ACT-Wazalendo**

siasa
JUMATANO FEBRUARI 21, 2024
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

EDWARD LOWASSA

# Baba na rafiki wa vyombo vya habari na taasisi zake

**Na Kajubi Mukajanga**



MARA nyingi nikifikiria urafiki kati ya vyombo vya habari na wanasiasa nakumbuka mchoro mashuhuri wa simba pamoja na swala, wameketi kama marafiki wanaopiga soga. Chini ya picha hiyo yapo maandishi: "Urafiki wa mashaka."

Kwa mwanasiasa mmoja ambaye nilimfahamu hakuakisi hali hiyo, alikuwa rafiki wa dhati wa vyombo vya habari ndiye Edward Lowassa, aliyefariki Jumamosi Februari 10, 2024 na kuzikwa nyumbani kwake Ngarash mwishoni mwa wiki iliyopita.

Nilimfahamu Lowassa miaka ya mwanzo ya 1990 akiwa mbunge na waziri, nami nikiwa mhariri wa gazeti la Wakati ni Huu. Lakini ushahidi wa kwanza muhimu niliouona katika uhusiano wake na vyombo vya habari ulikuwa mwaka 1997.

Alikuwa mtu wa kwanza kupeleka shauri katika Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa ajili ya utatuzi na usuluhishi. Tukio hili ni muhimu katika historia ya vyombo vya habari nchini maana MCT ndiyo ilikuwa imeanza kazi baada ya kupata usajili rasmi Mei 22, 1997 kufuatia kuundwa na wanahabari 30, Juni 1995.

Kesi ya Lowassa dhidi ya gazeti la Heko ilikuwa ni mtihani muhimu kwa asasi hiyo changa iliyopigia upatu utaratibu wa vyombo vya habari kujisimamia vyenyewe (self-regulation).

Agosti, 1997 Heko ilichapisha habari kubwa ukurasa wa kwanza iliyodai kuwa Edward Lowassa na "vigogo wengine" walikuwa wametajwa katika ripoti ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Kero ya Rushwa, maarufu Tume ya Warioba ya Rushwa.

Itakumbukwa kuwa baada ya kuingia madarakani, Rais Benjamin Mkapa, aliunda tume iliyoongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu Joseph Warioba, kuchunguza mianya ya rushwa na kutoa mapendekezo.

Ikiwa na kichwa cha habari: Tume ya Kero ya Rushwa: Baadhi ya viongozi, vigogo, ambao watafikishwa mahakamani wafahamika: Yumo ... Lowassa ... na wengineo, gazeti lilidai kuwa katika ziara ya mkoani Ruvuma Mkapa alikuwa ameahidi kuwa wote waliotajwa na Tume ya Warioba wangefikishwa mahakamani na kwamba gazeti lilikuwa limebaini kuwa mmoja wao ni Lowassa.

Katika malalamiko yake mbele ya Kamati ya Maadili ya MCT, Lowassa alisema habari hiyo ilikuwa ya uongo, ilimchafua, pamoja kuwasiliana na gazeti hilo limekataa kumsafisha.

Lowassa alidai gazeti lilikuwa na "ajenda ya siri" dhidi yake kwa kuwa lilikuwa na mtindo wa kuandika habari za kashfa dhidi yake yakiwamo madai kuwa alikuwa ametumia Shilingi milioni 50 kwenye kampeni mwaka 1995.

Alisema licha ya Profesa Rwekaza Mukandala wa Kamati ya Kufuatilia Uchaguzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye gazeti lilimtaja kama chanzo chao kukanusha habari hiyo, bado Heko haikurekebisha wala kuomba radhi kwa taarifa hiyo.

Pamoja na kwamba Lowassa angeweza kwenda mahakamani ambapo ikiwa angeshinda angelipwa fidia kubwa ya pesa, au kulalamika kwa waziri wa habari (mkubwa mwenzie) ili achukue hatua kwa mujibu wa Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, aliamua kwenda MCT, taasisi ambayo ilikuwa haijawahi kusikiliza shauri lolote, na ambayo ilikuwa imeundwa na wanahabari hao hao anaowalalamikia.

Ni imani hii katika mfumo huu mpya, wa wanahabari kujisimamia wenyewe, ambayo inaifanya kesi hii kuwa ya kihistoria.

Kamati ya Maadili ya MCT iliyokuwa na jukumu la kusikiliza malalamiko ya wajumbe wake walikuwa wanasheria wawili na wanahabari watano, iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba, makamu wake Dk. Sengondo Mvungi.

Wengine walikuwa waandishi Lawrence Kilimwiko, Salim Said Salim, Jenerali Ulimwengu, Marie Shaba na Danford Mpumilwa.

Kwa kuwa mwenyekiti wa Kamati alikuwa mtu yule yule aliyeongoza tume inayosemekana ilimtaja Lowassa kama mmoja wa wala rushwa, Jaji Warioba alijiondoa usikiliza shauri hilo, akimwachia makamu wake Dk. Mvungi. Katibu Mtendaji wa Baraza akiwa Anthony Ngaiza.

Shauri lilisikilizwa Septemba 23, 1997, uamuzi uliofikiwa na kamati ukawa gazeti lilikiuka vipengele kadhaa vya Kanuni za Maadili za Wanataaluma ya Habari, likaamriwa kuomba radhi na kulipa fidia ya usumbufu ya Shilingi 1,000,000 ambazo Lowassa alitaka zipelekwe kwa vituo vya watoto yatima. Mchapishaji wa gazeti hilo, Ben Mtobwa, alikubali na kutekeleza maamuzi hayo na shauri likafungwa.

Shauri hili liliipa MCT umashuhuri na uhalali mbele ya wadau wa habari, na muhimu wananchi, ambao walianza kupeleka malalamiko yao walipochukizwa au kuumizwa na mwenendo wa vyombo vya habari. Watu wakajua kwamba badala ya kwenda mahakamani kutumia fedha na muda mwingi, kulikuwa na chombo ambacho kingeweza kusikiliza mashauri na kuyatolea maamizi au kuyasuluhisha bila gharama kubwa na kwa muda mfupi, halikuwa tukio pekee.

Lowassa alipeleka shauri jingine MCT kuhusiana na taarifa sita zilizochapishwa na gazeti la Dira ya Mtanzania kati ya Oktoba na Novemba 2011, zikimshutumu na kumtuhumu kwa mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuhujumu Rais Jakaya Kikwete na CCM mkoani Arusha na masuala ya uadilifu.

Kikao cha kusikiliza shauri hilo kilifanyika 20 Septemba 20, 2012 chini ya mwenyekiti Jaji Thomas Mihayo, lakini gazeti halikutokea, wala kutekeleza maamuzi ya kamati, pamoja na kwamba Lowassa angeweza kupeleka mashtaka mahakamani baada ya ukaidi wa gazeti, hakufanya hivyo, akisema malalamiko yake yalikuwa yamesikilizwa na chombo cha tasnia na kutolewa maamuzi ni kwake hiyo ilitosha.

Hata hivyo, baadaye Kamati ya Maadili ya MCT ilipotembelea ofisi za Msama Promotion na Dira Company Limited, wamiliki na wachapishaji wa gazeti hilo, Mkurugenzi Alex Msama, alikiri makosa na kuonyesha mshtuko kwa jinsi mambo yalivyokuwa yakien-

INAENDELEA UK. 14

HOFU MIAKA MIWILI VITANI

# Urusi, Ukraine waelekea kupigana bila mwisho



Marais Volodymyr Zelensky wa Ukraine na Vladimir Putin wa Urusi. **PICHA ZOTE:MTANDAO,**

**Mwandishi Wetu**

JUMAMOSI wiki hii, Urusi inatimiza miaka miwili tangu ilipoivamia Ukraine kivita, ikitaka kupanua utawala wake kwa kuiweka nchi hiyo jirani chini ya himaya yake.

Vita hivi vilivyoanza Februari 24, 2022 baada ya Rais wa Urusi, Vladimir Putin, kutuma msafara mkubwa wa vifaru wa kilometa 64 uliofuatiwa na ule wa magari ya kivita siku tatu baadaye uliokuwa na urefu wa kilomita 15.5.

Si zana hizo tu, Putin alituma wanajeshi 200,000 nchini Ukraine akitazamia kuumiliki mji mkuu wa Kyiv na kuiangusha serikali ya Volodymyr Zelensky, katika muda wa siku chache.

Ripoti za vyombo vya habari vya kimataifa pamoja na picha za satelaiti zilionesha kwamba msafara wa magari ya kijeshi ulifikia urefu wa kilometa 56 Februari 29, 2022.

Wanajeshi wa Urusi wakavurumisha mizinga na makombora kuelekea Ukraine, wakavunja majengo muhimu na kuharibu makazi pamoja na miundombinu na wakafanikiwa kupata 'ushindi' wa haraka ambao haukufanikiwa kutimiza lengo la msingi la kuimiliki nchi hiyo.

Lengo la kuangusha serikali ya Zelensky, halijafanikiwa kwa miaka miwili sasa licha ya kwamba vikosi vya Urusi viliteka haraka maeneo makubwa, vimeshindwa kuizunguka Kyiv.

Wadadisi wa siasa za kimataifa wanaona kwamba Putin ni kama ameshindwa kwa kuwa lengo lake halikuwa kupigana kwa miaka miwili bali kwa saa au siku chache na kuweka serikali ya Kyiv mikononi mwake.

Swali la kujiuliza ni kwa nini nguvu kubwa kama hiyo ilishindwa kufika Kyiv?

Taarifa zinaonesha kwamba kadiri siku zilivyozidi kusogea, vikosi vya Putin vilipoteza maeneo vilivyoyadhibiti na hadi Desemba 2022, vilikuwa vimepoteza zaidi ya nusu ya sehemu zilizotekwa mwanzoni mwa uvamizi.

Mathalani, Urusi iliteka mikoa minne ya Ukraine mwishoni mwa Septemba na hadi Desemba 2022, iliipoteza.

Mkazi wa eneo la Bucha, Kaskazini mwa Kyiv, Volodymyr Scherbynyn, anasema asubuhi ya Februari 24, 2022 alikuwa amesimama nje ya duka lake, wakati msururu wa magari ya kivita zaidi ya 100 yakitokea Urusi kuingia nchini mwao.

Ripoti mbalimbali za BBC kuhusu mzozo huo ziliwanukuu watu wa kada tofauti wakiwamo wanajeshi, idara za ujasusi za kitaifa na kimataifa na raia ambao walikutana na msafara wa magari na vifaru vya Februari 24, 2022.

Taarifa za kijasusi zinaeleza kuwa Ukraine ilitulia kwa nia ya kumsoma na kuelewa mpango wa Urusi, kabla ya kutuma wanajeshi wake vitani.

**MPANGO PUTIN**

Taarifa zinaonyesha kwamba pamoja na ripoti nyingi za vyombo vya habari wakati huo, msafara wa vifaru na magari yenye silaha za vita, ulikuwa na vikosi 10 tofauti vya Kirusi, kulingana na kikosi cha wanajeshi cha Ukraine.

Mkakati wa Putin ulikuwa baada ya kikosi cha kwanza kuvuka hadi Ukraine saa 4:00 asubuhi Februari 24, vilitakiwa visonge mbele moja kwa moja hadi Kyiv ikifika saa 8:55 mchana.

Mipango hiyo inaelezwa kwamba ilipaswa kufanywa kwa usiri na kasi hata hivyo zilipita saa, zikawa siku, ikawa miezi na sasa ni miaka miwili bila Ukraine kuwa chini ya Urusi.

Wanajeshi wa Ukraine wakaanza kuudhibiti msururu huo kwa kushambulia baadhi ya magari jambo ambalo lilipunguza kasi ya msafara huo.

Wadadisi wanaozungumza na vyombo vya habari vya kimataifa kwa nyakati tofauti wanaeleza kuwa uvamizi huo ni mkubwa zaidi wa Ulaya tangu mwisho wa Vita vya Pili vya Dunia.

Licha ya kuwaacha mamilioni ya Waukraine bila makazi, mara kadhaa Rais Putin amekaririwa akisema kuwa huo si uvamizi wala vita bali ni 'operesheni maalum ya kijeshi.'

Putin amekuwa akisema kuwa lengo ni kuizuia Ukraine kuwakaribisha maadui wa Urusi na ndio sababu za kutuma wanajeshi Kaskazini, kusini na mashariki, alipoanza hicho anachoita 'operesheni ya kijeshi.'

Adui anayetajwa na Urusi hapa Umoja wa Majeshi ya Kujihami (NATO) yenye mkono mrefu wa nchi za Magharibi hasa Marekani.

Mwezi mmoja baada ya uvamizi, Putin alitangaza kukamilika kwa awamu ya kwanza na kuwarudisha nyuma wanajeshi wake kutoka karibu na Kyiv na Chernihiv na kujipanga tena.

**ATHARI ZAIDI**

Vita hivyo vimetajwa kutikisa uchumi wa dunia na vimeumiza zaidi nchi maskini. Vimeharibu njia za usambazaji bidhaa na kutatiza mifumo mikuu ya usafirishaji hasa baada ya kuteka jiji la bandari lililoharibiwa la Mariupol huko Donetsk katikati ya Mei, 2022.

Utekaji huo uliviongezea nguvu vikosi vya Putin ambavyo vilipata ukanda wa ardhi kutoka mpaka wa Crimea, rasi ya Ukraine iliyotekwa na Urusi mnamo 2014.

Taarifa zinaonesha kwamba vikosi hivyo vilifanikiwa pia kunyakua ardhi kwenye pwani ya Bahari Nyeusi kuelekea eneo lililojitenga la Moldova.

Ripoti za kimataifa zinaonesha kuwa hadi Oktoba 2022, jeshi la Moscow chini ya Jenerali Sergei Surovikin, lilibadili mkakati wake kwa kuharibu miundombinu ya kiraia ya Ukraine, kuharibu asilimia 40 ya mfumo wake wa umeme na kutekeleza mashambulizi ya anga nchini kote.

Lengo la Kremlin lilikuwa kupunguza ari ya raia na ndio maana alipiga miji kote Ukraine.

**SILAHA ZA MAREKANI**

Msaada wa silaha za kivita hasa makombora ya Himars ya Marekani kwa jeshi la Ukraine, kuliathiri vituo vya vifaa vya Urusi na maghala ya silaha yaliyokuwa yanatekeleza vita.

Septemba 2022, Putin alitangaza usajili wa wanajeshi wa akiba 300,000 kwa lengo la kuimarisha vikosi vyake hasa vya Mashariki. Wiki kadhaa baadaye, Urusi ilijiondoa kutoka kwa mji wa Kherson, mji mkuu wa kikanda pekee uliotekwa katika vita vyake vya 2022.

**UPUNGUFU URUSI**

Wachambuzi wa vita hivyo, wanaeleza kuwa kupotea kwa jiji la Kerson na kurudi nyuma kwa wanajeshi 30,000 wa Urusi kutoka ukingo wa kulia wa Mto Dnipro, kulifunika changamoto za Urusi kwenye uwanja wa vita na kuleta picha pana ya uvamizi uliojaa kushindwa.

Ukraine ilipata ushindi wa ishara kwa kuzama kwa meli ya jeshi la wanamaji la Urusi katika Bahari Nyeusi huko Moskva.

Wiki kadhaa baadaye wanajeshi wa Urusi walilazimika kukimbia kambi ndogo ya Kisiwa cha Snake katika Bahari Nyeusi. Hata hivyo, Rais Putin hajakata tamaa pamoja na kwamba jumuiya ya kimataifa imemtaka arejee kwenye meza ya mazungumzo.

**Kwa mujibu taarifa kimataifa**

UNAPOGONGA HODI UCHAGUZI…

# Mwenyekiti CCM Tanga atumia mtaji wa Rais, Makonda kuwasha moto uwajibikaji

## • Amwiga kukosoa, kugharamia; asindikizwa na Kibajaji



Mwenyekiti wa CCM Tanga, Rajabu Abdallah, akimkaribisha Mbunge Sonia Magogo, CCM baada ya kuitema CUF, akieleza 'kukoshwa' na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye mkutano wilayani Handeni. Anayecheka kulia ni Mbunge wa Handeni Mjini, Reubine Kwagilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu, HANDENI**

MIAKA miwili ya uchaguzi, hesabu na joto zake zimeanza, mwaka uliopo kukitarajiwa Uchaguzi wa Serikali za Mtaa, huku unaokuja ndio 'baba lao' Uchaguzi Mkuu 2025. Kisiasa 'asiye na mwana aeleke jiwe.'

Wakati vyama kama ACT-Wazalendo vikiendeleza wajibu wake na siasa kukosoa utendaji wa serikali kila hatua, CHADEMA inaendesha maandamano iliyoruhusiwa kuwasilisha inayodai, jana yakiwa ya tatu jijini Mbeya, baada ya Dar es Salaam na Mwanza; kote ni majiji kitaifa.

Mkongwe CCM, anajitetea anajikosoa na kujipanga. Hapo kuna ziara kila kona ya nchi za Komredi Paul Makonda, Katibu wa Itikadi na Uenezi na Mafunzo, akikosoa na kuweka sawa utendaji wa serikali wanayoisimamia, baada ya kushinda uchaguzi uliopita. Alianza nayo, aliyekuwa Katibu Mkuu, Komredi Daniel Chongolo.

Ni aina ya ziara inayoacha darasa, hatua na kuunda jambo la kichama katika sura moja ya utendaji kitaifa; dhana ya uwajibikaji wa serikali kwa wananchi waliowapa dhamana kupitia masanduku ya kura.

### MKOANI TANGA

Itakumbukwa Makonda akiwa ziara za ukaguzi mkoani Tanga mwezi uliopita, ikaripotiwa kubainika kasoro za migogoro ya kijamii na kiserikali, akalazimika kumpigia simu waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, namna alivyokuta migogoro wilayani Pangani na mapendekezo ya hatua kichama.

Pia, ikaendana na maagizo kwa wenyeviti wa CCM katika wilaya mbalimbali kuwasilisha kasoro za kiutendaji za Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs), kuhusu utendaji ulivyo, ili wenye kasoro wachukuliwe hatua.

Ni kwa vipi wenyeji mkoani wanaendeleza? Hapo Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Komredi Rajabu Abdallah, ana ufafanuzi wake katika ziara na matendo staili ileile ya Makonda, akinena:

"Viongozi wote wa chama (CCM) kuanzia vijiji hadi wilaya na hata wa ngazi ya mkoa, ni wakati huu wa kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwenyekiti wetu taifa, kwa kuhakikisha tunatatua changamoto wanazokumbana nazo wananchi badala ya kukaa maofisini."

Ni kauli yake Komredi Abdallah, katika ziara staili ya Makonda, wilayani Handeni, Tanga mwezi huu, ikiwa ni wiki kadhaa baada ya Katibu Mwenezi wa CCM Taifa kuzuru.

Abdallah akiwa katika mkutano wa hadhara Viwanja vya Chanika, akaibuka na mazao kisiasa 'akimvuna' aliyekuwa mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama Cha Wananchi (CUF), Sonia Magogo, kuhamia CCM, akiwa na baadhi ya wafuasi wake 25.

Sonia alikuwa Mbunge wa Viti Maalum, CUF kutoka mkoani Tanga kati ya mwaka 2015-2020, pia akagombea ubunge jimbo la Handeni mjini, mwaka 2020, akiwatamkia mkutanoni 'wananchi wa Handeni walimwonyesha ushirikiano mkubwa."

Katika uchaguzi huo, Sonia kupitia CUF akapata kura 6,713, huku Reuben Kwagilwa wa CCM akashinda kwa kura 15,241.

"Kazi kubwa anayoifanya mheshimiwa Rais Wetu wa Jamhuri, imenisukuma leo kuja kuungana nanyi ili tuongeze nguvu kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele kwa kumuunga mkono mama yetu Samia.

"Kwa dhati kabisa naomba nimpongeze Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga kwa namna anavyojitahidi kukijenga chama chetu hiki, ambacho nimetangaza kujiunga nacho kwa sababu ni sehemu salama kwangu," akatamka.

Hapo napo Mbunge wa Handeni Mjini, Reubine Kwagilwa, akajinasibu kuwa hatua ya mshindani wake Sonia kurudi CCM, ni ishara kwamba wilaya yao haina tena upinzani.

### YA MAKONDA TANGA

Ziara za Mwenyekiti wa CCM Mkoa Tanga, zina unasaba wa staili na kinachojiri kwa viongozi wa juu wa CCM, akiwamo Katibu Mwenezi Makonda kwenye ziara mikoa mbalimbali, ambako kila anakopita anawasilishiwa na idadi kubwa ya kero anazowasilishiwa kutoka utendaji kiserikali.

Hapo kumekuwa kukikosolewa na sura ya ombwe la kiongozi katika mikoa mbalimbali, kutokana na wananchi kukosa pa kuwasilisha kero zao, badala yake wakisubiri viongozi wa kitaifa, jambo ambalo ni hatari kwa uhai wa chama.

Inasisistizwa, ni wakati wa kuanza kutenda kuanzia ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya ambako kuna viongozi wa chama ambao ndio jukumu lao kuisimamia serikali, hivyo wananchi wakasikilizwa na kutatuliwa kero zao kama sababu ya msingi wa wananchi kukiamini chama hicho.

Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa CCM - Tanga, Abdallah, anasema kumekuwapo kasumba za watendaji na watumishi wa chama kukaa ofisini, badala ya kwenda mitaani kutatua changamoto za wananchi.

Anasema ni hali inayosababisha wananchi hao kusubiri watendaji wa juu wa chama, lisilopaswa kufumbiwa macho, katika hatua za kumuunga mkono Rais Dk. Samia, anadumu katika harakati za kuwakwamua Watanzania.

"Naomba viongozi wenzangu tumuunge mkono mwenyekiti wetu kwa kushuka huku chini ambako watu wanahitaji kutatuliwa shida zao kama dhamira ya chama chetu kilichoaminiwa kushika madaraka ya kuliongoza Taifa.

"Tukifanya hivi tutakuwa tunamuunga mkono Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa kwa vitendo, kwa sababu tumetatua kero na shida za wananchi wetu ambao kwa namna moja ama nyingine hakuna wa kuwakomboa isipokuwa serikali ya chama chetu," anatamka.

### AWEKEZA MAMILIONI

Abdallah akiwa kwenye uzinduzi wa shina la wajasiriamali wa Kijiji cha Kibaya, Kata ya Misima, katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, anatoa shilingi 4,000,000, kuchangia ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho.

Ni mchango wake, baada ya kuguswa na kinamama waliowasilisha kwa viongozi, wakiomba wajengewe zahanati, kupunguzia adha ya kufuata huduma ya afya.

Mwenyekiti akaahidi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya ujenzi wa zahanati hiyo, akiwataka wataalamu wa wilaya, viongozi wa chama na wananchi kwa pamoja kushirikiana kwa karibu katika mradi wa ujenzi huo.

"Nimetoa fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Kibaya, hivyo lazima mfahamu mimi ni mfuatiliaji mzuri. Nikitoka hapa nataka shughuli za ujenzi zianze ili kuwakomboa wananchi wanaoteseka juu ya suala zima la afya," akatamka.

Katika ziara hiyo, pia akasindikizwa na mbunge wa Mtera, Livingstone Lusinde maarufu 'Kibajaji' ambaye mbali na kutoa hotuba zilizofurahisha wengi, pia alichangia mifuko 50 ya sementi kukamilisha zahanati ya Kibaya.

# Ndivyo moto wa 50/50 unavyowaka ACT-Wazalendo

## •Kinamama wakijitosa uongozi wa juu, kamati

**Na Halfani Chusi**

WANAWAKE wa Chama cha ACT Wazalendo wamejitokeza kwa wingi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa chama linapofunguliwa dirisha la kuchukua fomu mwezi huu.

Itakumbukwa kuwa kiongozi wa kwanza wa chama hicho ni mwanamama Anna Mughwira (sasa marehemu) aliyekuwa mwenyekiti na kiti chake kukaliwa na Zitto Kabwe.

Licha ya kuhamia CCM na kuteuliwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, kinamama wa ACT-Wazalendo wanaendelea kufuata nyayo zake, safari hii wakijitokeza kuwania uenyekiti na pia ujumbe kwenye kamati mbalimbali.

Makamu Mwenyekiti Taifa Bara, Dorothy Semu, anajitosa kuwania nafasi ya kuwa kiongozi wa chama ambayo kwa sasa ni jahazi linaloendeshwa na Zitto.

Anaponadi sera zake, anaiambia Nipashe kuwa atasimama imara ili chama hicho kibaki kuwa sauti ya Watanzania zinapotokea changamoto mbalimbali.

"Kitakuja na sera mbadala zinazotekelezeka na kujibu shida za wananchi pamoja na kuwaunganisha kuwa kitu kimoja."

Anaendelea kujinadi kuwa atasaidia kuwafanya viongozi wao kuwa bora na kufanya chama hicho kuwa mfano, akisisitiza kwamba anataka kukifikisha kwenye ushindi utakaoweka rekodi.

"Nimeamua, ninaamini kwenye uongozi wa pamoja nimekitumikia chama hiki kwa miaka nane katika majukumu mbalimbali, wakati wa misukosuko ya kidemokrasia, kilipotishiwa kufutwa nilisimama tulishirikiana na kuhakikisha kinapata hati safi." Anasema Dorothy.




Husna Sungura, mgombea wa ujumbe wa Kamati Kuu Kanda ya Pwani. **PICHA ZOTE: HALFAN CHUSI**




Waziri Mkuu Kivuli wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu.

Anaongeza:"Ninaamini kwenye uongozi wa pomoja ninaona sasa ni wakati wa kuchukua nafasi hii kubwa, kwa kuwa haijawahi kuwa wazi nahisi ninatosha na ninafaa kulipeleka jahazi hili mbele," anatamba mwanamama huyu ambaye ni Waziri Mkuu Kivuli.

Anakumbusha kuwa amekuwa Waziri Mkuu na wafuasi wa chama chao wameona jinsi alivyoweka kipaumbele masuala ya Watanzania katika matatizo mbalimbali na kuchochea uwajibikaji serikalini ili kufikia maisha bora kwa wote.

"Ninaomba ridhaa kwenye uchaguzi Machi nipate kura nyingi niwe kiongozi wa pili kukiongoza chama hiki, kwa miaka 10 iliyopita tumeendelea kutengeneza viongozi katika kila nyanja. Sina shaka nitapata timu njema itakayopeleka chama hiki kwenye ushindi na kushika uongozi wa nchi," anaongeza.

Dorothy anasema amefikia uamuzi huo, baada ya tafakari ya kina na uamuzi usio na shaka, kwamba anaweza kusukuma gurudumu hilo kama alivyoshika nyadhifa nyingine za kuongoza na kutetea chama.

Anaeleza kuwa dhamira yake inatokana na mambo matatu mosi, uongozi wa pamoja, utumishi wa watu na kuonyesha njia ili kutimiza kwa ukamilifu malengo makubwa ya ACT- Wazalendo.

"Mmenipima kwenye majukumu mbalimbali kwa miaka hii nane, baada ya kuwa mtumishi wa umma kwa miaka 17. Nitaje machache. Nilipokuwa Katibu Mkuu 2017-2020 nimekivusha chama kwenye mawimbi makubwa ya ukandamizaji wa kidemokrasia."

Anasema Dorothy na kufafanua kuwa jambo lililokikumba chama hicho lilikuwa ni kufutiwa usajili wakati wa awamu ya tano.

Anasema ameweka historia kwa ACT-Wazalendo kuvuja rekodi za usimamizi wa kifedha na kuwa chama kinachokua kwa kasi kuliko vingine Afrika.

"Nikiwa Makamu Mwenyekiti Bara 2021 nilipewa jukumu jingine la kukaimu uenyekiti wa chama baada ya kifo mwenyekiti wetu mpendwa Maalim Seif Shariff Hamad na kuhakikisha anapatikana mwenyekiti mwingine kwa mfumo wa kidemokrasia kama matakwa ya katiba yetu," anaongeza.

Anaahidi kutumia uzoefu na karama ya uongozi kuliongoza jahazi la ACT-Wazalendo hatimaye kushika hatamu za kuiongoza Tanzania.

Anasema jambo la pili, anaamini katika wajibu mkubwa wa vyama shindani na kwamba uwapo wa chama hicho katika siasa za vyama vingi umeendelea kutoa changamoto na maana halisi ya wajibu wa vyama kujenga demokrasia na siasa za ushindani.

Dorothy anasema anataka nafasi hiyo ili kuendeleza dhima ambayo chama hicho kimeibeba kwa miaka 10 sasa na matumaini inayotoa katika uongozi wa nchi hii.

"Ninataka kuongoza ndoto hii ya ACT-Wazalendo kufikia mabadiliko chanya, ya kweli, ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Nafasi nilizowatumikia za Katibu wa Sera na Utafiti na sasa Waziri Mkuu Kivuli zimeendelea kunipika na kunipa uzoefu mkubwa ndani na nje ya chama na taifa."

"Ndugu zangu uongozi ni kujitoa, kufanya kazi kwa bidii na maarifa, kutimiza majukumu na malengo ya chama na maslahi ya Watanzania," anasisitiza Dorothy.

Anaeleza kuwa sera zao, zinasadifu kile wanachotamani kukifanya, zimejawa na uchu wa kufikia maendeleo kwa ajili ya chama na taifa na kuleta mapinduzi ya wanawake katika uongozi ACT-Wazalendo na hata kutimiza lengo la uwiano wa 50/50.

Pamoja na kuwania nafasi hiyo ya juu Dorothy anaungana na Husna Sungura, anayewania anayelenga kuwa mjumbe wa Kamati Kuu Kanda ya Pwani.

Anajinadi kuwa anayo historia ya kukibeba chama hicho katika harakati za uchaguzi na kufikia ushindi mkoani Kigoma.

Husna anasema ni mwanachama tangu 2015 akikumbushia kuwa kutokana na mahaba kwa ACT-Wazalendo, alipambana na hata kuacha shughuli za chama Pwani na Dar es Salaam, na kuweka nguvu zaidi Kigoma ili kuhakikisha ushindi unapatikana.

"Sikula, sikulala usiku, nilitembea kutwa mlango kwa malango, nilijitoa hivyo kwa mapenzi makubwa ya chama changu, nilianzisha kampeni ongea na nduguyo, hii ilifanikisha ushindi kwa wana ACT waliokuwa mbali na Kigoma na nje ya nchi," anakumbusha Husna.

# BABA NA RAFIKI WA VYOMBO VYA HABARI, TAASISI ZAKE

**INATOKA UK. 11**

delea katika ofisi yake.

Badala ya kuchukua njia za kuvishtaki vyombo vya habari kwa mkondo wa mahakama, Lowassa ni mwanasiasa ambaye alichagua njia ya usuluhishi pale alipoona ametendewa visivyo.

Urafiki usio wa mashaka wa Lowassa kwa vyombo vya habari ulijidhihirisha pia kwa matendo mengine. Wakati kikundi cha waandishi kilipoanzisha Kampuni ya Habari Corporation iliyochapisha magazeti ya Mtanzania, Rai moja ya changamoto iliyopata ilikuwa ni ofisi.

Lowassa aliahidi kuwasaidia na mara chama cha ukombozi wa Afrika Kusini cha Pan Africanist Congress of Azania (PAC) kilipohama kutoka ofisi zake zilizokuwa mtaa wa Mkwepu katikati ya jiji la Dar es Salaam, Lowassa, akiwa Waziri wa Ardhi, alihakikisha Habari Corporation inapata ofisi hapo.

Hata katika safari zake za kikazi, alihakikisha wanahabari wanakuwapo. Japo kama mwanasiasa yeyote makini naye alitaka kutangazwa, lakini alielewa umuhimu wa wananchi kujua serikali yao inafanya nini kupitia vyombo vya habari.

Nilipokuwa mhariri wa Wakati Ni Huu miaka ya mwanzoni ya 1990 na yeye akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu tulichapisha habari kadhaa "nyeti" zilizogusa maslahi ya wafanyakazi wa usalama wa taifa.

Tulishafahamiana na nilijua habari hizo zilikuwa zikimsumbua. Lakini tulipokutana, alichoniambia ni: "Kajubi, unapata wapi habari hizo zisizokanushika?"

Mwaka 1995 nchi ilipokuwa katika joto kubwa la uchaguzi wa vyama vingi baada ya miongo kadhaa, nilifanya mahojiano maalum na aliyekuwa mkuu wa majeshi, Jenerali Robert Mboma. Msingi wa mada ya mahojiano yetu ulikuwa nafasi ya jeshi katika mfumo wa vyama vingi. Hata hivyo, baadaye yalikwenda katika mambo mbalimbali na baadhi yakagusa watu wakubwa jeshini.

Gazeti lilipotoka na habari hizo ikawa "kizaazaa"! Ni wazi, kuna watu wenye nguvu ambao hawakufurahia habari zile. Zilikuwa taarifa mbili au tatu, zote ukurasa wa kwanza.

Ndipo msaidizi wa Lowassa, Saidi Nguba, alipokuja ofisini Sinza na kunipa wito wa Lowassa, akitaka kuzungumza nami kesho yake asubuhi.

**KUITIKIA WITO**

Ilikuwa Jumamosi, nikaenda ofisini kwake akiwa Waziri wa Ardhi. Alikuwa mcheshi sana, na hatimaye akaleta suala la taarifa ile iliyohusu masuala ya matumizi ya wakubwa, ambayo chanzo nilikuwa nimekihifadhi.

Yeye hakugusia habari kuu, ambayo nilishapata lawama kutoka kwa wakubwa wengine kwamba mahojiano yangu yalikuwa yamewajenga wapinzani. Jenerali alikuwa amezungumza kwa kirefu na akahitimisha kwamba jeshi litaheshimu maamuzi ya wananchi bila kujali wamechagua chama au mgombea gani.

Lowassa akanifahamisha kuwa baadhi ya wakubwa jeshini walikuwa wamechukizwa sana na taarifa hiyo kuhusu matumizi. "Shida ni kwamba haikanushiki," akaniambia, na kuongeza, "Na inaonekana chanzo chako ni cha juu."

Nikakaa kimya. "Kwa hiyo ni chanzo cha juu mno," akadadisi. "Unajua siwezi kuzungumzia chanzo changu kilichonipa habari," nikamjibu. Basi nitayamaliza. Watu wanasema mambo ya kutisha. Nashauri kuwa hiyo stori uliyoandika inatosha. Usijihatarishe."

Tukaendelea na maongezi mengine, lakini nilikuwa na mshtuko, na nikapata funzo. Nilikuwa mhariri, lakini uzoefu wangu haukuwa mkubwa sana. Nikajifunza kuwa kila chanzo cha habari kina sababu ya kukupatia taarifa kinazokupa. Ni juu ya mhariri kufanya maamuzi ya kitu gani atumie.

Lowassa alipenda waandishi na vyombo vya habari. Alipoteuliwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 1990 aliamua msaidizi wake awe mwandishi wa habari, akamchukua Saidi Nguba kutoka Uhuru na Mzalendo.

Hata alipohamia Wizara ya Ardhi alihama naye na baadaye alipokuwa Waziri Mkuu alimchukua katika nafasi ya Mwandishi wa Waziri Mkuu.

Nguba anaarifu kuwa Lowassa alikuwa chanzo cha habari kizuri kwa wahariri wengi, aliwapa taarifa hata habari kubwa au 'scoop' ambayo haijachapishwa wala kutangazwa popote. Aliwapenda na kuwathamini wanahabari na kila wakati alikuwa tayari kuongea nao na kuwasaidia.

**Mungu aiweke pema roho ya marehemu Edward Lowassa.**



# HABARI DODOMA

## Vijana, wazee washauriwa kupima tezi dume kila mara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI Bingwa wa Mifumo ya Mkojo pamoja na Uzazi kwa Wanaume katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Dk. Frederick Mabena, amesema kutokana na tishio la ugonjwa wa tezi dume, vijana na wazee wajenge utaratibu wa kupima afya zao waonapo dalili.

Ametaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni mtu kwenda haja ndogo zaidi ya mara tatu usiku, lakini pia kujisaidia haja ndogo bila kipimo.

Bingwa huyo alisema kundi hilo linapaswa kufanya hivyo pindi waonapo dalili ya ugonjwa huo ili kupata matibabu mapema.

"Ninaomba watu kuzingatia suala hili, matibabu yanapatikana katika Hospitali ya Benjamin Mkapa wanapoona dalili hizi waje, kuna madaktari bingwa wa matatizo haya, watu wasione aibu kwenda kupata matibabu,"alisisitiza.

Hata hivyo, alisema hivi sasa wamekuwa wakitoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na tezi dume kwa kuzingatia masuala ya vyakula wanavyokula ikiwamo kufanya mazoezi.

"Watu wengi wanaokumbwa na tezi dume mwisho huwasababishia kupata saratani ya tezi na figo kufeli au kupata Anemia,"alisema.

Bingwa huyo alisema ugonjwa huo unatibika kama ilivyo kwenye magonjwa mengine, hivyo jamii isione haya waende kwa wataalam wa afya ili kupata matibabu.

## Wanane mbaroni madai kuuza sukari kinyume cha bei elekezi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Bodi ya Sukari Tanzania wamefanya msako jijini hapa na kukamata wafanyabiashara wanane waliobainika kuuza sukari kinyume na bei elekezi iliyotolewa na serikali.

Ofisa Mwandamizi Bodi hiyo, Fahiri Achi, akizungumza jana kuhusu msako huo, alisema wafanyabiashara hao wamekaidi maelekezo ya serikali ya kuuza bidhaa hiyo kwa bei elekezi.

"Operesheni hii ni ya nchi nzima na hapa Dodoma tumebaini wafanyabiashara wasio waaminifu waliopandisha bei ya sukari na kuuza kinyume na bei elekezi, watahojiwa na Jeshi la Polisi,"alisema.

Achi alisema wafanyabishara hao wanauza sukari ya kilo 50 kwa Sh. 190,000 hadi 200,000 wakati bei elekezi ni Sh. 140,000.

"Kwa kilo 25 za sukari wanauza kwa Sh. 105,000 hadi 110,000 wakati bei elekezi ni Sh. 70,000 lililotolewa na serikali kwenye tangazo namba 40 ya mwaka 2023, Bodi ilitoa maelekezo mahsusi ya kusimamia bei elekezi,"alisema.

Achi alisem katika msako huo wamebaini sababu za kutokushuka bei ni wafanyabiashara wa jumla wa kati wananunua sukari kwa wasambazaji wakubwa ambao wanaficha bidhaa hiyo katika stoo zao na kugeuka kuwa wafanyabiashara wa rejareja.

"Tumeona wanaweka sukari kwenye mifuko ya kilo moja hadi tano ili wauze kwa kilo moja Sh. 4,400 hadi 5,000, kitu ambacho ni mzigo kwa wananchi na serikali haitafumbia macho suala hili.

"Mmeona kuna mfanyabiashara yule 'Mhindi' amenunua kwa Gulamali kwa Sh. 140,000 sukari kutoka India, lakini yeye anauza Sh. 190,000, kitu ambacho si sawa, Bodi tutasimamia suala hili kuhakikisha wananchi wanauziwa kwa bei halali iliyotangazwa na serikali, "alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa. Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Abdalah Hassan Mitawi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## UWT yahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), umeanza kujipanga kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu na kuwaasa wanawake wajitokeze kugombea nafasi za uongozi.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Mary Chatanda, aliyasema hayo jana jijini hapa katika semina ya kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya UWT kuhusu masuala ya kijinsia.

Mary alisema viongozi waliopo kwa sasa katika vijiji na mitaa, wanawake ni wachache ndio maana wamejipanga kutoa hamasa kwao kushiriki ipasavyo katika chaguzi kwa kugombea nafasi za uongozi.

"Tumedhamiria safari hii lazima kuwa na wanawake wengi katika nafasi za uongozi ngazi za kijiji, mtaa, kitongoji. Niombe wanawake wa vyama vingine twende tuondoe mambo ya vyama tukasimamie wanawake waingie kwenye uongozi,"alisema.

Mary alisema kamati hiyo itawapa mbinu za kuwaelimisha wanawake wengine ili kujua kuna chaguzi hizo na wajibu wao kujitokeza kugombea.

"Tumejipanga safari hii kwa sababu tuna Rais mwanamke, Spika mwanamke. Tuna kila sababu ya kutia msukumo kwa wanawake, ni wakati wetu sasa wa kujitokeza kwa kila mwanamke mwenye uwezo wa kugombea ajitokeze,"alisisitiza.

Akizungumzia ziara za UWT, Mary alisema wamekutana na kero mbalimbali zinazohitaji utalaamu wa kisheria.

"Sisi tunaanzisha kitengo cha sheria hapa makao makuu ili wanawake waliopata changamoto na kuhitaji msaada wa kisheria wasaidiwe.

"Kamati hii itafanya kazi hiyo chini ya uongozi wa Mbunge wa Viti Maalum, Zainab Katimba,"alisema.

Alibainisha kuwa katika kukiimarisha kitengo hicho watatafutwa vijana wanawake waliosoma sheria na wanaopenda kusaidia jamii katika mikoa ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya UWT ya Haki na Sheria, Zainab Katimba, alisema mafunzo hayo yanatolewa na wadau mbalimbali wa masuala ya jinsia ikiwamo Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF).

## Wanajeshi TZ walioshiriki vita Uganda waomba kifuta jasho

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANAJESHI wa Tanzania walioshiriki vita vya Uganda kuanzia 1978 hadi 1979 wameiomba serikali kuwalipa kifuta jasho kutokana na kushiriki vita hivyo.

Aidha, wameupongeza Umoja wa Afrika (AU) kwa kuweka sanamu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere katika Makao Makuu ya Ofisi hizo yaliyoko Mji wa Addis Ababa, nchini Ethiopia.

Mmoja wa wanajeshi hao, Frank Maghoba, akizungumza na waaandishi wa habari jana, alisema suala la kuwekwa sanamu hiyo linapaswa kwenda sanjari na kuwalipa wanajeshi walioshiriki vita hivyo ambapo ni zaidi ya miaka 40.

Alisema hawajalipwa haki zao licha ya serikali ya Uganda kuahidi kuwalipa kifuta jasho kutokana na kushiriki vita hivyo.

Alisema kilichofanywa na AU ni kutambua namna Mwalimu Nyerere alivyoshiriki katika ukombozi wa Bara la Afrika ambaye alitaka bara lote liwe huru, ambapo katika kufikia malengo hayo, walitumika wanajeshi wa Tanzania kupigana.

"Rais Samia Suluhu Hassan, wanajeshi wengi tulioshiriki vita hivyo hususan Uganda na kufanikiwa kumng'oa nduli Idd Amini, ambaye alivamia ardhi ya Tanzania hatujalipwa wakati sisi tulikuwa tunafanya kazi hiyo kwa kutii amri ya Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania ambaye ni Rais Julius Nyerere kipindi hicho," alisema Maghoba. Maghoba ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Kigamboni jijini Dar es Salaam, alisema kila mwaka wanajeshi walioshiriki vita hivyo vya Uganda wamekuwa wakiitwa kwenye ofisi za Wakuu wa Wilaya kujaza fomu za kumbukumbu na kuahidiwa kulipwa jambo ambalo halijatekelezwa hadi sasa.

"Rais Samia wanajeshi wengi wamekufa bila kupata haki yao wakati wanastahili kupata asante yao kutoka serikali ya Uganda ambayo inadaiwa ilishatoa fedha hizo. Nchi zingine zinaheshimu wanajeshi wake hasa waliofanya kazi ya kulinda heshima ya nchi zao," alisema Maghoba.

Katika uzinduzi wa sanamu hiyo juzi, Rais Samia alisema hiyo inadhihirisha mchango mkubwa wa Mwalimu Nyerere katika ukombozi, umoja na amani ya Afrika na fahari ya Bara la Afrika katika urithi wake mkubwa.



# Afa maji akitoa gurudumu kwenye dimbwi

Na Elizabeth John, NJOMBE

MTOTO Cosmas Gadau (13), mkazi wa Mtaa wa Kisiwani, ulioko Kata ya Kivavi Halmashauri ya Mji Makambako mkoani Njombe, amefariki dunia baada ya kudumbukia katika dimbwi la maji wakati akichukua gurudumu alilokuwa anachezea.

Tukio hilo lilitokea Februari 17, mwaka huu, saa 12 jioni katika Mtaa wa Igangidung'u ambako mtoto huyo alishindwa kutoka kwa sababu ya kina kirefu cha dimbwi hilo.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Igangidung'u, Emmanuel Gadau, alisema tukio hilo lilitokea wakati mtoto huyo alipokuwa anaendesha tairi la baiskeli na kuingia ndani ya dimbwi hiyo.

Alisema baada ya tukio hilo mtoto huyo alivua nguo na kuingia katika dimbwi hilo ili aliitoe bila kujua kama lina kina kirefu.

"Tukio hili limeniuma niwaombe wazazi wawaelekeze watoto maeneo ya kucheza na hususani msimu huu wa mvua kubwa. Ukiona huelewi mtoto alipo ni vema ukajua mtoto yuko wapi," alisema Gadau.

Mwenyekiti huyo alisema dimbwi hilo lilisababishwa na watu ambao wanachimba mchanga kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao.

Alisema kifo cha mtoto huyo ni cha pili kutokea kikifuatiwa na cha mtoto mwingine kilichotokea mwaka jana.

Baba mzazi wa marehemu, God Gadau, alisema alipokea taarifa za kifo cha mtoto wake kutoka kwa baadhi ya wanandugu na kutoa ushauri kwa serikali kuzuia wananchi kuchimba mchanga katika makazi ya watu ili kuepuka vifo vya aina hiyo.

"Ninaomba serikali kuchukuwa hatua juu ya madimbwi yote ambayo yapo mtaani na yanayochimbwa kwa sababu ya matofali, wanachimba mchanga kwa ajili ya kupigia lipu. Mimi yametokea, tusipochukua hatua yatazidi kutokea kwa mwingine," alisema Gadau.

Baadhi ya wananchi wa Mtaa wa Igangidung'u na Kisiwani, Daniel Mkongwa, Ahabu Madete na Ayubu Chaula, walisema katika maeneo yao kuna madimbwi mengi yanayosababishwa na shughuli za kufyatua tofali na kuchimba mchanga.

"Ombi langu vijana wanaojihusisha na shughuli za uchimbaji mchanga waangalie mazingira, wasichimbe katika vina virefu ambavyo vinasababisha athari kwa watoto wetu," alisema Mkongwa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kivavi, Daria Kilasi, aliwataka wananchi kuachana na tabia ya kufyatua tofali na kuchimba mchanga wa ujenzi katika mkazi ya watu kwa sababu hali hiyo inasababisha uharibifu wa mazingira.

"Tunaendelea kuwasisitiza wananchi wetu wasiendelee kuchimba mashimo hata kama wanafyatua tofali wawe wanasawazisha sio kuweka mashimo makubwa," alisema Kilasi.



Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo (kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa kampuni ya kutengeneza vifaa vya umeme ya Elsewedy Kigamboni Dar es Salaam, wakati Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilipotembelea kiwanda hicho, juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

MGAWO WA UMEME

# Wasafiri hadi Malawi kusaga nafaka

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WANAWAKE wa Wilaya ya Kyela, mkoani humo wanalazimika kusafiri kwenda kusaga nchini Malawi kutokana na kukatika katika kwa umeme wilayani humo na hivyo kusababisha mashine nyingi kushindwa kufanya kazi.

Mbunge wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Mbeya kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Suma Fyandomo, aliyasema hayo juzi katika Kikao cha Bodi ya Ushauri ya Barabara (Road Board) kilichofanyika juzi mkoani hapa.

Aliiomba serikali kushughulikia haraka tatizo la kukatika kwa umeme akidai kuwa, kitendo cha wananchi kwenda kusaga nafaka nchi jirani kinasababisha usumbufu na ni mateso kwao.

"Najua kikao hiki hakihusiani na masuala ya umeme, lakini ninaomba nikitumie kufikisha kilio cha wanawake wenzangu wa Wilaya ya Kyela, wamekuwa wakinipigia simu mara kwa mara wakilalamikia kukatika kwa umeme.

"Wanasema wanakwenda kusaga nchini Malawi, ninakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidie pia kuongeza msukumo," alisema Fyandomo.

Alisema kitendo hicho pia, kinasababisha kudumaza uchumi wa wananchi kwa maelezo kuwa, wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta huduma hiyo ya umeme nchi jirani badala ya kufanya kazi za kujiingizia kipato.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alisema hivi karibuni walijadili tatizo hilo katika Kikao cha Halmashauri Kuu na kumwagiza Waziri kushughulikia haraka tatizo hilo.

Alisema walikubaliana kwamba, ajenda ya mgawo wa umeme na upungufu wa sukari ni miongoni mwa ajenda ambazo zimekuwa zikisumbua na hivyo, mawaziri wanaohusika walipewa maelekezo maalumu.

"Tunaomba wananchi mvute subira hili tatizo linakwenda kuisha hivi karibuni. Tulimuelekeza Waziri ashughulikie haraka sana tatizo hili la umeme na ninaamini litakwisha muda sio mrefu," alisema Mwaselela.

Hata hivyo, Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alipokuwa anawasili mkoani Mbeya kwa ajili ya kuanza ziara ya kikazi, alisema tatizo la umeme nchini linashughulikiwa na litamalizika hivi karibuni baada ya miradi ya kimkakati kumalizika.

Alisema kwa sasa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere uko mbioni kuanza kuzalisha nishati hiyo na kwamba, ndio unaotegemewa kumaliza tatizo hilo na hata vyanzo vingine vinaendelea kushughulikiwa.

Alisema hivi karibuni mradi huo umeanza kufanyiwa majaribio na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea kushughulikia tatizo hilo.

"Tunaendelea kushughulikia tatizo hili na muda sio mrefu litakwisha, lile Bwawa la Mwalimu Nyerere litaongeza uzalishaji wa umeme kwa kiasi kikubwa kwa hiyo Gridi ya Taifa itaongezeka ufanisi," alisema Dk. Biteko.

Biteko yuko mkoani Mbeya kwa lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uchorongaji wa visima vya maji moto wilayani Rungwe kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa umeme kwa kutumia chanzo cha joto ardhi.

## BRELA yashtuka wamiliki leseni hatarini kushtakiwa kwa ugaidi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), umeanza kutoa mafunzo maalumu kuhusu sheria ya umiliki wa kampuni ili kuwaepusha wamiliki kuingia katika makosa ya uhalifu wa kifedha ikiwamo utakatishaji fedha, kufadhili ugaidi na usafirishaji haramu wa fedha.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi jijini Mbeya kwa maofisa mbalimbali wanaosimamia sheria wakiwamo wanasheria, mahakimu, maofisa wa jeshi la polisi, Jeshi la Uhamiaji, maofisa wa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Kaimu Mkurugenzi wa Usajili wa Majina ya Biashara wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA), Isdor Nkindi, alisema walianzisha mafunzo hayo baada ya mabadiliko ya sheria ya umiliki wa kampuni ambayo yalianza kuwatambua baadhi ya wadau ambao sheria na kanuni za awali zilikuwa haziwatambui.

Alisema baadhi ya wadau hao ambao ni wamiliki manufaa walikuwa hawaonekani katika nyaraka za usajili wa kampuni hali ambayo wakati mwingine walikuwa wanajikuta wanaingia kwenye matatizo ambayo walikuwa hawajui.

Alisema kwa sasa sheria inawataka wanufaika hao wa kampuni ambao awali walikuwa hawatambuliwi kusajiliwa kwenye daftari tofauti na wanufaika wengine.

"Tunatoa mafunzo haya kwa sababu dhana hii ya umiliki manufaa katika kampuni ni mpya na tunawaelimisha wamiliki ili wawatambue wafadhili wao na wasikubali kufadhiliwa na watu wasiowajua ili wasiingie kwenye matatizo ya uhalifu wa kifedha," alisema Nkindi.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa siku tano mfululizo mkoani humo na kwamba, baada ya kumaliza kwa wadau hao, wataanza kuyatoa kwa wamiliki wa kampuni na baadaye wataingia mitaani kuwasaidia wananchi kufungua kampuni zao.

Alisema wanawasikiliza wadau wao wote wanaoshiriki katika urasimishaji wa biashara ili wajue matatizo ambayo wanakutana nayo katika kazi yao na kujadiliana namna ya kuyakabili.

Baadhi ya wadau walioshiriki mafunzo hayo walisema, kuna mambo ambayo yamekuwa yakifanyika katika kampuni, lakini walikuwa hawajui kama yanaweza yakasababisha uhalifu wa kifedha.

Emelda Aluko, ambaye ni mwakilishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, alisema wamekuwa wakiendesha kesi mbalimbali za uhalifu wa kifedha ikiwamo utakatishaji fedha, lakini walikuwa hawajui baadhi ya mazingira ambayo kesi hizo zinatokea.

Alisema kupitia mafunzo hayo walifundishwa namna ambavyo uhalifu huo unaweza ukafanyika katika kampuni na ukamsababishia mtu matatizo hayo.

Alisema kupitia mafunzo hayo walielewеshwa kuwa, kuna baadhi ya watu kampuni zao zinaweza zikatumika kufanya uhalifu huo bila wao wenyewe kujua.



## Serikali yaweka takwimu za parachichi kutoka nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali ina takwimu za uzalishaji na uingizaji wa zao la parachichi kutoka nje ya nchi kupitia bandari visiwani humo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Prof. Omar Fakihi Hamad, aliyetaka kujua takwimu kuhusiana na zao hilo na uingiaji wake Zanzibar.

Shamata alisema uzalishaji wa zao hilo umefikia tani 26,093 ambapo kwa mwaka jana, Unguja ilikuwa na tani 11,782 na Pemba tani 14,311.

Alisema uingizaji wa zao hilo kutoka nje ya visiwa hivyo umefikia tani 609,358.935 kwa mwaka 2023.

"Mheshimiwa Spika, hapana na hakuhitajiki utafiti wa kimazingira kwa zao hili ambalo kiasili ni zao la kitropiki kama yalivyo mazao ya embe, fenesi na matunda mengine," alisema.

Alisema parachichi limekuwa likilimwa na kustawi katika maeneo yote ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa.

Waziri Shamata alisema serikali imejitayarisha kuhamasisha wakulima kulima parachichi ili kuongeza tija ya kiuchumi na kiafya kwa kuwaelimisha wakulima kuingia kwenye kilimo cha parachichi kwa kupanda zao hilo kibiashara.

Hata hivyo, alisema serikali imekuwa na kawaida ya kuotesha na kuwauzia miche wakulima kila mwaka, ambapo kwa mwaka 2023 jumla ya miche 4,400 parachichi imeoteshwa na kupandwa katika mashamba ya wananchi ambapo miche 1,800 ni vitalu binafsi na 2,600 vya serikali.

# Zanzibar kununua sukari kiwandani kudhibiti bei

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itanunua sukari inayozalishwa katika Kiwanda cha Sukari Mahonda ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kupanda bei ya bidhaa hiyo.

Kwa sasa bei ya sukari kwa kilo imefikia Sh. 3,000 wakati bei elekezi ya awali ya serikali ni Sh. 1,800 kwa kilo.

Akizungumza na uongozi wa kiwanda hicho jana baada ya kufanya ukaguzi wa uzalishaji wa sukari huko Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema bei ya sukari imepanda.

Alisema kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) imeamua kuchukua hatua hiyo ili kurahisisha upatikanaji wake hasa katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambacho bidhaa hiyo inatumika kwa wingi.

"Matumizi ya sukari huongezeka zaidi katika mwezi wa Ramadhan na unakaribia, hivyo ni vyema tukazalisha kwa wingi na kutegemea sukari ya kwetu kuliko kusubiri kutoka nje ya nchi," alisema. Waziri Shaaban alisema serikali itaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano katika kiwanda hicho ili kuhakikisha uzalishaji unaongezeka na kuleta tija kwa wananchi wa Zanzibar.

Aidha, alisema kuwa, dhamira ya serikali ni kuhakikisha bidhaa hiyo inayozalishwa haitoki nje ya Zanzibar ili kuondosha malalamiko ya wananchi yanayotokana na kupanda kwa bei.

"Sukari iliyokuwapo ndani ibaki hapa hapa kwetu, kuna baadhi ya watu wanatoka nje ya Zanzibar kufuata sukari huku na kusababisha wananchi kukosa bidhaa hii," alisema waziri huyo.

Naye Meneja Rasilimali Watu kutoka Kiwanda hicho cha Sukari Mahonda, Bashiru Wazir Muhamed, alisema wanatarajia kuzalisha tani 5,000 endapo hakutakuwa na mvua ambayo itaathiri uzalishaji.

Alisema kutokana na hali ya kuwapo kwa mvua uzalishaji huo umeanza Februari 9, mwaka huu, jambo ambalo lililosababisha kuchelewa kuanza.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania, Fatma Mohamed Abdallah (wa pili kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Elimu, Maandalizi na Msingi Zanzibar, Fatuma Mode (kushoto) na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, wakikata utepe kuzindua majengo ya Shule ya Msingi Kisiwandui jana, baada ya kampuni hiyo kufanya maboresho ya majengo na madarasa na ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miti ya mpingo, misandali yatajwa hatarini kutoweka

**Na Rahma Suleiman,** aliyekuwa BAGAMOYO

MITI ya asili ya mpingo, misandali na mikurungu imetajwa kuwa hatarini zaidi kutoweka kama juhudi za makusudi hazitachukuliwa katika kulinda na kuhifadhi misitu ambayo ni rasilimali muhimu nchini.

Ipo hatarini kutokana na kushambuliwa kwa kasi katika misitu ya hifadhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo za uvunaji wa mbao na mkaa.

Ofisa Mhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Reuben Magandi, aliyasema hayo jana wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari ya namna ya kukabiliana na uhalifu haramu wa misitu.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kupitia Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Alisema miti hiyo ipo hatarini kutoweka kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo uvunaji wa mbao na mkaa usiozingatia hali ya uhifadhi wa mazingira.

"Tanzania inafaidika sana na miti hiyo inalindwa na Mkataba wa Kimataifa wa CITES wa Mwaka 2014 na miti hii endapo itatoweka uharibifu wa mazingira utaendelea na nchi kubaki kuwa jangwa," alisema. Aidha, alisema juhudi mbalimbali zinafanyika katika kurejesha uoto wa asili na TFS kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali na wananchi wanahamasisha upandaji wa miti na kutoa miche ya mimea mbalimbali kwa wananchi na shuleni ili kuipanda ambayo inasaidia katika uhifadhi wa mazingira.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu ya kutunza uoto wa asili na kulinda maliasili kwa jamii zinazoishi kwenye mapitio ya wanyama pori (shoroba) katika hifadhi za maliasili.

Pia alisema kuwapa miche ya kupanda bure na hutoa elimu ya biashara kupitia misitu hiyo ikiwamo ufugaji nyuki na uvunaji asali ili waone umuhimu wa kuitunza.

"Tumesaini mikataba ya kimataifa na kushirikisha taasisi zingine zinazolinda mimea ambayo ipo hatarini kutoweka kwa ajili ya kuilinda isivunwe kiholela," alisema.

Akizungumzia changamoto za uharibifu wa mazingira, Makandi alisema katika misitu ya hifadhi moto ni hatarishi na ili kukabiliana nao huwashirikisha wananchi katika kujua sababu ya miti ya asili kuungua.

Alisema wamekuwa wakiwapatia elimu ya kulinda miti hivyo kusaidia kulinda misitu isiiungue moto. Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema wanahabari ni wadau muhimu katika kuelimisha umma katika suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira na wanapaswa kutoa taarifa kuhusu bayoanuai kwa wananchi katika kutunza na kuhifadhi.

Alisema JET imekuwa ikitoa mafunzo kwa waandishi wa habari tangu mwaka 1991 ilipoazishwa na ni endelevu kwa sababu bado baadhi ya waandishi hawajafikiwa na mafunzo ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Alisema kwa sasa JET inatekeleza Mradi wa Tuhifadhi Maliasili unaofadhiliwa na Mradi wa USAID Tuhifadhi Malialisi Tanzania ambao ni wa muda wa miaka mitano na unaangazia shoroba saba Tanzania.

Waandishi wa habari walipatiwa mafunzo hayo, waliahidi kuyatendea kazi kwa kuuhabarisha umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa kuwa yanapoathirika athari mbalimbali hujitokeza ikiwamo mabadiliko ya hali ya hewa.

Jumla ya waandishi wa habari 20 wamepatiwa mafunzo hayo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambao wamejumuisha kutoka vyombo vya serikali na binafsi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SIMA CONSTANTINE SIMA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE455322** iliyotolewa mnamo Tarehe 04/02/2022 makao makuu DAR ES SALAAM PCO. Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DOD/DOD/4952/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba, Kituo cha Ibwera Mkoa wa Kagera**

**Shauri la Madai 02/2024**

**Jina la Mdai....................STANSLAUS ZACHARIA**

**Jina la Mdaiwa ...............JACKLINE FERDINANDI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa JACKLINE FERDINANDI,** Kwa kuwa mdai ameleta madai ya pesa shilingi 380,000, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 28 Mwezi 2 Mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili, ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 7 Mwezi 2 Mwaka 2024.

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(TANGA DISTRICT REGISTRY)**
**AT TANGA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.8 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AZIZI SELEMANI HAMED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR PROBATE BY NASSIRI AZIZI SELEMANI**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of the probate Rule)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioners.

The petition has been fixed for hearing on 28th Day of February, 2024 before **Hon. M. CHABA, J.**
Objections to the grant should be filed on or before the **28th day of February, 2024.**

Dated at Tanga this **09th Day of February, 2024**

Deputy Registrar
TANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 06/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KWIRINI NGALASON TAIRO wa DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MAGRETH KWIRINI TAIRO**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 Mwezi 03 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 19 Mwezi 02 Mwaka 2024.

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**CRIMINAL APPEAL**

**CAUSE NO. 813/2024**

**ASHA YOHANA.................................APPELLANT**

**VERSUS**

**WINFRIDA GAUCHO........................RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention/Hearing on **28th day of FEB 2024 at 08:30 a.m. Before Hon R. KASELE PRM**
**YOUR ARE** require to appear in this Court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.

Given under my hand and the seal of the Court this 20th day of FEB 2024

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

**COPY TO BE SERVED UPON**
**WINFRIDA GAUCHO**

---

**FORM 58**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**
**IN THE COURT OF DSTRICT DELEGATE OF ARUSHA/ARUSHA DISTRICT COURT**

**AT ARUSHA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 63 OF 2023**

**In the Metter of the Estate of the Late............DOROCELLA FERDINAND KAHWA**

**And**

**In the Matter of an Application Letters of Administration of the late....................... DOROCELLA FERDINAND KAHWA**
**By................................................ ROBERT OPIYO MAUDI**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of NOVEMBER 2023.
The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the court .
Dated at Arusha this 20th day of NOV 2023

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.2344 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE THERESIA ALOYCE KILAVI**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**1. SALIM JUMANNE MOGELA**
**2...........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of 03 /2024.
Dated at Morogoro this 14 day of 02/ 2024.

Resident Magistrate

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Wakazi wa Gaza wakiwa wameinamisha vichwa ishara ya kukosa matumaini kuhusu operesheni za Israel zinazoendelea katika ukanda huo. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yaendelea kuishambulia Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

ISRAEL imeishambulia tena Gaza na kutoa amri kwa wananchi ya kuondoka katika baadhi ya maeneo ya ukanda huo, wakati mataifa makubwa yakishughulishwa na namna ya kufanikisha usitishaji vita kabla ya kura ya UM.

Ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yalifanyika jana na kusababisha zaidi ya Wapalestina milioni 2.2 kwenye ukingo wa njaa na robo tatu ya watu kuyakimbia makazi yao, kwa mujibu wa makadirio ya Umoja wa Mataifa (UN).

Mataifa makubwa yanayojaribu kutafuta njia ya kuondoka kwenye mzozo huo unaotishia kusambaa yanapanga kuwasilisha azimio katika Baraza la Usalama, kushinikiza usitishaji vita, huku mataifa yote ya Umoja wa Ulaya (EU) isipokuwa Hungary, yakitoa wito wa kusitisha vita mara moja kwa sababu za kiutu.

Pia yamehimiza Israel kutouvamia mji wa kusini mwa Gaza wa Rafah, ambako Wapalestina karibu milioni 1.5 wanajihifadhi.

Mji huo ambao ndiyo wa mwisho usioguswa na majeshi ya ardhini ya Israel, ndiyo pia lango kuu la misaada inayohitajika sana kupitia nchi jirani ya Misri.

Kwa mujibu wa Shirika la Wakimbizi wa Kipalestina la Umoja wa Mataifa (UNRWA) mashambulizi ya Israel dhidi ya mji huo yanatatiza operesheni za kiutu, huku ugavi wa chakula ukivurugwa na ufungaji wa mara kwa mara wa mpaka.

Shirika hilo pia lilieleza kuwa uhaba wa chakula na maji umewaacha watoto na wanawake kote katika ukanda huo wakikabiliwa na ongezeko kubwa la utapiamlo.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) linasema mtoto mmoja kati ya sita kaskazini mwa Gaza sasa wana utapiamlo, hali ambayo inaelekea kuzidisha kiwango ambacho tayari hakivumiliki cha vifo vya watoto.

Licha ya wito wa mara kwa mara wa kuiepusha Rafah, Israel imetoa muda wa hadi kufikia mwezi wa Ramadhani kwa Hamas kuwaachilia mateka wanaowashikilia vinginevyo itaendelea na uvamizi wa ardhini.

Mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Vita, Benny Gantz, alisema "Ikiwa kufikia Ramadhani mateka hawatakuwa nyumbani, mapigano yataendelea kila mahali ikiwamo eneo la Rafah."

Wapatanishi wa kimataifa wamekuwa wakihangaika kuepusha mashambulizi hayo na mauaji yanayohofiwa ya raia wengi, huku kukitolewa mapendekezo mawili ikiwamo iliyoandaliwa na Algeria, inadai kusitishwa mara moja kwa mapigano kwa misingi ya kibinadamu na kuachiliwa bila masharti kwa mateka wote.

Andiko hilo, lililoonekana na AFP Jumatatu, linasisitiza uungaji mkono wa usitishaji mapigano kwa muda huko Gaza kwa haraka iwezekanavyo, likielezea wasiwasi kwa kuonya kwamba mashambulizi makubwa ya ardhini yatasababisha madhara zaidi kwa wananchi na uhamaji.

Kulingana na chanzo cha kidiplomasia, rasimu hiyo pia ina nafasi ndogo ya kupitishwa kama ilivyoandikwa, na ina hatari ya kupigiwa kura ya turufu na Russia.

Wakati Marekani imeshinikiza makubaliano ya kusitisha vita kwa ajili ya kuwaachiliwa mateka, mazungumzo ya wiki kadhaa yanayohusisha wapatanishi wa Marekani, Misri na Qatar yameshindwa kufikia makubaliano.

Wakati huo huo ilielezwa kuwa Hamas imetishia kujiondoa katika mazungumzo hadi pale msaada zaidi utakaporuhusiwa kuingia Gaza, huku Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu akikataa matakwa ya Hamas na kuyataja kama ndoto.

Ilielezwa kuwa ilipinga vikali wito wa majadiliano kujumuisha kutambuliwa kwa taifa la Palestina. "Tunakataa kabisa hili, itahatarisha uwepo wa taifa la Israel."

Mwishoni mwa juma, waandamanaji wa Israel walijaribu kuzuia malori ya misaada katika mpaka wa Misri na Gaza ili kuongeza shinikizo la kuachiliwa kwa mateka.

Mjini Jerusalem, waandamanaji waliandamana hadi kwenye nyumba ya Netanyahu, wakimtuhumu kwa kuwatelekeza mateka.

"Hakuna njia nyingine ya kuwarudisha watu hawa bila makubaliano," alisema mwandamanaji Eli Osheroff. **DW**

# Rais Macky Sall aridhia uamuzi wa baraza la katiba

**DAKAR,** SENEGAL

KWA mujibu wa barua iliyolifikia shirika la habari la (AFP) Rais wa Senegal, Macky Sall, amesema kwamba dhamira yake ni kuheshimu uamuzi wa baraza la katiba na atafanya mashauriano yanayohitajika kuandaa uchaguzi huo wa mapema iwezekanavyo.

Aidha, inaelezwa kuwa kutokana na siku kadhaa za maandamano nchini humo serikali imeamua kuwaachilia huru wafungwa 300 na kwamba wengi walioachiliwa ni watu waliokuwa wamezuiliwa jela baada ya kukamatwa na vikosi vya usalama wakati wa maandamano.

Nchini Senegal sakata la kuahirishwa uchaguzi linaendelea kufukuta, huku mashirika ya kiraia nchini humo yakitaka uchaguzi ufanyike kabla ya muhula wa Rais Macky Sall haujakamilika mwezi Aprili, mwaka huu.

Pia ilielezwa kuwa wagombea wengine 15 wa urais kati ya 20 wanataka uchaguzi huo ufanyike Aprili 2 na sio baada ya hapo.

Rais Macky Sall bado anakabiliwa na shinikizo kutoka kila upande kuhusu hatua yake ya kuahirisha uchaguzi uliokuwa umepangwa kufanyika tarehe 25 mwezi huu. Jana Jumatatu wagombea 15 walisaini barua inayotaka tarehe ya uchaguzi na tarehe ya rais Macky Sall kuachia ngazi zisiwe Aprili 2.

Mamlaka za nchi hiyo zilipiga marufuku maandamano huku zikifanyika operesheni maalum za Jeshi la Polisi na kukamatwa kwa wanaharakati wa upinzani, pamoja na kuzuia huduma zote za mawasiliano kwa njia ya mtandao.

Akizungumza na DW, mwanaharakati wa masuala ya kiraia Nina Penda, alisema ameshusha pumzi kutokana na hatua mpya za kisiasa zinazochukuliwa akisema kwamba anafurahi sana kuona wafungwa wa kisiasa kuachiwa huru.

Ilielezwa kuwa wiki iliyopita baraza la katiba lilibatilisha hatua hiyo ya rais, huku majaji wa baraza hilo wakipitisha uamuzi kwamba Desemba 15 iliyotangazwa kama siku ya uchaguzi mpya wa bunge nayo ni kinyume cha sheria na sio halali.

Hata hivyo ilielezwa kuwa mashinikizo hayo ndiyo yaliyomfanya Rais Macky Sall kutoa tamko akisema kwamba yuko tayari sasa kufuata uamuzi huo uliotolewa.

Tangu uchaguzi ulipoahirishwa hakuna harakati zozote za kampeni zinazofanyika nchini humo na wanasiasa wengi wa upinzani wamekamatwa kutokana na maandamano. **DW**



HABARI MICHEZO

# CHIPUKIZI WAWAZUIA KMKM KUWASHUSHA JKU SC KILELENI

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM SC imeshindwa kukata kiu yake ya kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Chipukizi FC ya Kisiwani Pemba.

Katika mchezo huo uliochezwa juzi katika Uwanja wa Mau A ni mzunguko wa 19 wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

KMKM SC ambayo ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 38 ingeshinda mchezo huo ingefikisha alama 41 na ingefanikiwa kumshusha JKU SC ambayo ndio kinara wa ligi hiyo ikiwa na alama 40.

Mchezaji wa Chipukizi FC, Faki Mwalimu, ndiye aliyezamisha manuari ya timu yake ya zamani, KMKM katika dakika ya 72 baada ya kupiga shuti lilotokana na mpira wa adhabu na kujaa wavuni.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema walikuja na mipango ya kupata ushindi, lakini mpango wao haukufanikiwa.

Alisema wachezaji walicheza vizuri katika kipindi chote cha dakika 90 na kwamba hata goli lililofungwa lilikuwa la bahati mbaya na si kama walizidiwa kiuchezaji.

Alisema tangu hapo awali alifahamu kuwa wanaenda kukutana na mchezo mgumu kwa kuwa hata mzunguko wa kwanza walishindwa kuifunga timu hiyo katika uwanja wao wa nyumba, Finya Kisiwani Pemba.

Alisema hayakuwa matokeo ambayo walitarajia licha ya kuwa na mipango ambayo ingefanikiwa wangeendeleza matumaimi yao ya safari za ubingwa.

"Mchezo huu ulikuwa mgumu kwa upande wetu na ni mchezo ambao kila timu inahitaji matokeo, sisi kwetu ilikuwa tunaendelea na harakati zetu za kutaka kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi, lakini kupoteza mechi hii haina maana kama tumevunjika moyo, bado tunaendeleza mapambano," alisema.

Aidha, alisema anajipanga kuelekea mchezo wao wa mzunguko wa 20 dhidi ya timu ya Ngome FC Februari 29, mwaka huu, utakaochezwa Uwanja wa Mau A Unguja.




Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini, ambapo jana usiku walishuka Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kuvaana na Polisi Tanzania kwenye mechi ya Kombe la FA. Jumamosi wiki hii pia Yanga itaikaribisha CR Belouizdad ya Algeria kwenye mechi ya Kundi D ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

# Tigo yajipanga Kili Half Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mbio za Kilimanjaro Marathon zitakazofanyika Jumapili wiki hii mjini Moshi, Kampuni ya Tigo imesema tayari imekamilisha maandalizi ya mbio za nusu marathon 'Tigo Kili half Marathon'.

Kampuni hiyo ndio mdhamini mkuu wa mbio hizo za half marathon ambapo wamehakikisha huduma zote muhimu zinapatikana siku ya tukio hilo.

Akizungumzia mbio hizo, Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema kampuni hiyo imejipanga kuwahudumia wanariadha na wateja wa Tigo watakaofika kwenye mbio hizo za kimataifa.

„Tumejipanga kutoa huduma nzuri, kutakuwa na Wi-Fi Spots ya 4G ya bure kwa watu wote watakaofika kwenye Uwanja wa Ushirika na maeneo mbalimbali ya Moshi mjini hasa Moshi Club ambapo tamasha la Kili Marathon litafanyika," alisema Kinabo.

Alisema kwa ujumla maandalizi yote ya mbio hizo yamekamilika na wanategemea wageni wataanza kumiminika mkoani humo kuanzia leo.

Kampuni ya Tigo inayoongoza kwenye mapinduzi ya kidigitali hapa nchini, kwa mara nyingine imeendelea kudhamini mbio hizo za half marathon ambapo kwa mwaka huu zitafanyika Jumapili wiki hiii.

## Simba, Yanga zatakiwa umoja mechi kimataifa

**Na Shufaa Lyimo**

WATANZANIA wametakiwa kuachana na Usimba na Uyanga na badala yake waungane kwa pamoja kuziunga mkono timu hizo zinapoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto, ndiye aliyetoa wito huo Dar es Salaam jana wakati akizindua Duka la Vifaa vya Michezo la Relaxo.

„Ni wakati wa Watanzania kuachana na Usimba na Uyanga pale timu hizo zinapokuwa zinashiriki mashindano ya kimataifa ili ziweze kusonga mbele na kuweza kuipeperusha vema bendera ya taifa letu, alisema Kumbilamoto.

Aidha, alisema anaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa hamasa kwa timu za taifa, ikiwa ni juhudi zinazofanywa na Rais Samia.

Naye Balozi wa Klabu ya Simba, Salum Kikeke, aliwataka wanamichezo mbalimbali waiunge mkono timu hiyo ikiwa ni pamoja na kujitokeza kununua viatu katika duka hilo kwani vina ubora wa hali ya juu.

## Ihefu FC yaota nafasi ya nne

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuvuna pointi tatu dhidi ya Geita Gold FC, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Mecky Maxime, ameanza kupigia hesabu pointi sita katika michezo miwili iliyopo mbele yao, akiwa na ndoto ya kupanda hadi nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ihefu FC ipo nafasi ya 10 ikiwa na alama 19 na ikifanikiwa kuvuna pointi sita dhidi ya Kagera Sugar ugenini na nyumbani itakapoikaribisha Mashujaa FC, itakuwa na alama 25 kwenye nafasi ya tatu ikimshusha Coastal Union ambayo ina pointi 23.

Akizungumza na Nipashe jana, Maxime alisema wanahitaji kupambana kuvuna pointi sita, michezo miwili kufikia malengo yao ya kujiweka kwenye nafasi nzuri ya msimamo wa ligi.

"Vijana wako vizuri tunaendelea na maandalizi baada ya mchezo wetu na Geita Gold FC, tumerudi katika uwanja wa mazoezi kusahihisha makosa yetu, yasijirudie katika mechi zijazo ikiwamo na Kagera Sugar tukiwa ugenini," alisema kocha huyo.

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER KUMRITHI TUCHEL
ALIYEKUWA Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anachukuliwa kuwa chaguo la muda mfupi na Bayern Munich ikiwa wataamua kumfukuza Thomas Tuchel. **(Sky Germany)**

### PIA WANAMTAKA ALONSO
MABINGWA hao wa Ujerumani pia wanafikiria kumnunua Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool. **(Sky Sport)**

### BRUCE AWINDWA KOREA
STEVE Bruce ana nia ya kuwa kocha ajaye wa Korea Kusini baada ya Jurgen Klinsmann kutimuliwa wiki iliyopita, lakini pia anajumuishwa kwenye orodha za Klabu za Saudi Arabia. **(Mirror)**

### TEL AVUTIA MAN UNITED
MANCHESTER United inavutiwa na mshambuliaji wa Bayern Munich na Ufaransa, Mathys Tel mwenye umri wa miaka 18, huku wakala wake akikiri kwamba lazima „wazingatie chaguzi zote" msimu huu wa majira ya joto. **(90min.com)**

### REIJNDERS PIA ATAJWA
‚MASHETANI Wekundu' (Manchester United) pia wanamlenga kiungo wa AC Milan na Uholanzi, Tijjani Reijnders mwenye umri wa miaka 25, **(Football Transfers)**

### ZIRKZEE ANYATIWA CHELSEA
CHELSEA inamfuatilia mshambuliaji wa Bologna na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa klabu nyingi, ikiwa ni pamoja na Arsenal, Manchester United na Barcelona. **(TeamTalks)**

### WATKINS AFIKIRIWA ARSENAL
ARSENAL inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Aston Villa, Ollie Watkins, 28. **(Fichajes)**

### KIMMICH KUONDOKA BAYERN
KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 29, anatazamiwa kuondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu huu kwa sababu uhusiano wake na kocha, Thomas Tuchel, umevunjika. **(Bild - Via Germany)**

### ZANIOLO KUREJEA VILLA
ASTON Villa haina uwezekano wa kubadilisha mkopo wa Nicolo Zaniolo kutoka Galatasaray kuwa mkataba wa kudumu msimu huu wa majira ya joto, huku kiungo huyo wa kati wa Italia mwenye umri wa miaka 24, akitaka kurejea Serie A. **(Calciomercato)**

### NEWCASTLE YATAFUTA BOSI
MKURUGENZI wa soka wa Brentford, Phil Giles, Mkurugenzi wa zamani wa Michezo wa Monaco, Paul Mitchell na Kocha Mkuu wa zamani wa AS Roma, Tiago Pinto, wanatarajiwa kuchukua nafasi ya Dan Ashworth huko Newcastle United. **(I)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE SASA AKARIBIA KUMALIZANA NA MADRID

Klabu hiyo ya Hispania ina matumaini ya kukamilisha makubaliano siku za usoni, lakini...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid ipo kwenye mazungumzo na fowadi wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe juu ya kumsajili bila malipo msimu huu wa majira ya joto na wana matumaini ya kumalizana naye hivi karibuni, vyanzo vimeeambia ESPN.

ESPN iliripoti Alhamisi kwamba Mbappe ameifahamisha PSG kwamba ataondoka kama mchezaji huru mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu, baada ya kuamua kuwa mustakabali wake uko Real Madrid.

Madrid iliwasilisha ofa rasmi ya mkataba kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa mwezi uliopita, huku PSG wakiwa bado na matumaini ya kumshawishi nyota wao kubaki.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Madrid sasa wana matumaini ya kukamilisha makubaliano katika siku za usoni, lakini mkataba bado haujasainiwa, na maelezo kadhaa bado yanahitaji kufuatwa.

Mbappe alianzia benchi kwenye ushindi wa mabao 2-0 wa PSG dhidi ya Nantes kwenye Ligue 1 Jumamosi, kabla ya kuingia uwanjani na kufunga penalti dakika ya 78.

Pia alifunga katika ushindi wa 2-0 wa klabu hiyo ya Ufaransa dhidi ya Real Sociedad katika mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Fowadi huyo amefunga jumla ya mabao 32 katika michuano yote msimu huu, licha ya kuwapo kwa tetesi kuhusu mustakabali wake.

Mbappe amekuwa akilengwa zaidi na Madrid kwa muda mrefu, na baada ya kuwa kwenye ukingo wa kumsajili mwaka 2022 - kabla ya mabadiliko yaliyomfanya Mbappe kusaini mkataba wa nyongeza PSG - lakini sasa wababe hao wa LaLiga wapo karibu zaidi kumchukua mshindi huyo wa Kombe la Dunia.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA AMUOMBA RADHI PHILLIPS

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ameomba radhi kwa Kalvin Phillips kwa kusema kuwa kiungo huyo alikuwa na uzito mkubwa aliporejea kutoka Kombe la Dunia la 2022.

Guardiola aliwaambia waandishi wa habari kwamba Phillips hakuwa katika hali nzuri ya kufanya mazoezi baada ya kurejea kutoka Qatar, ambako alitumiwa kwa dakika 40 pekee katika mechi mbili za akiba kwenye kikosi cha England.

Phillips alivumilia wakati mgumu akiwa City baada ya kusajiliwa kutoka Leeds United mnamo 2022, alianza mechi sita pekee ndani ya miezi 18, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 28, alijiunga na West Ham United kwa mkopo mwezi uliopita.

Baada ya kuhamia West Ham, kiungo huyo alisema kujiamini kwake kumepata "pigo kubwa" kutokana na matamshi ya Guardiola.

"Ndiyo, samahani," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari kuhusu kumuomba radhi Phillips

"Ninaomba msamaha kwake. Nilizungumza naye kabla ya kutoa maoni. Sijawahi, huwa sizungumzi na timu kabla sijasema kitu hapa, au mchezaji katika kesi hiyo."

City, ambao wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wanaweza kupunguza pengo la viongozi Liverpool hadi pointi moja kama jana, Jumanne walishinda mchezo wao dhidi ya Brentford nyumbani.



## Solskjaer awaniwa kumrithi Tuchel Bayern

**MUNICH, Ujerumani**

OLE Gunnar Solskjaer amezingatiwa kama chaguo la kujaza nafasi kama kocha wa muda pale Bayern Munich ikiwa Thomas Tuchel atafukuzwa, kwa mujibu wa Sky Sport.

Tuchel anakabiliwa na shinikizo kubwa pale 'Bavaria', ambapo Bayern iko katika hatari ya msimu wa kwanza bila taji tangu 2011/12, kutokana na kufungwa mara tatu mfululizo.

Sky Sport imeeleza kwamba, Solskjaer kocha wa zamani wa Manchester United ndiye anayepewa nafasi kubwa zaidi kama Tuchel atafukuzwa, ingawa miamba hao wa Ujerumani bado wana nia ya kumweka bosi wao wa sasa katika nafasi ya kumpa nafasi ya kubadilisha mambo.

Solskjaer alishinda mechi 91 kati ya 168 akiwa kocha wa Man Utd, baada ya hapo awali kufurahia vipindi viwili vya kuinoa miamba ya Norway, Molde na Cardiff City.

Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Christoph Freund, anamfahamu Solskjaer vema na inasemekana amekuwa karibu naye sana kwa miaka mingi raia huyo wa Norway.

Pia kuna nia ya mchezaji wa zamani wa Ufaransa, Zinedine Zidane, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu kama kocha Real Madrid.

Kufungwa kwa Bayer Leverkusen na Bochum kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kumeifanya Bayern kushuka kwa pointi nane nyuma, huku wakihitaji kupindua kipigo cha mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora na Lazio baada ya matokeo duni na kusababisha sare 1-0.

Leverkusen kwa sasa inanolewa na Xabi Alonso, ambaye pia anatajwa kuwa shabaha ya Bayern.



## Napoli yamfukuza kocha wao

**NAPLES, Napoli**

KLABU ya Napoli imemfuta kazi kocha Walter Mazzarri baada ya kuifundisha kwa miezi mitatu pekee na nafasi yake kuchukuliwa na Kocha wa Timu ya Taifa ya Slovakia, Francesco Calzona.

Mazzarri alimrithi Rudy Garcia mnamo Novemba mwaka jana baada ya kuwa na mwanzo mbaya kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Taarifa kutoka nchini Italia zinaeleza kuwa Calzona amesaini mkataba hadi mwishoni mwa msimu huu na ataendelea kuinoa Timu ya Taifa ya Slovakia.

Mmiliki Aurelio de Laurentiis alimshukuru Mazzarri kwa "kuisaidia timu katika kipindi kigumu".

Napoli inawakaribisha Barcelona katika mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumatano.

Calzona aliteuliwa kuwa KOCHA wa Slovakia mnamo Agosti 2022 na kusaidia taifa hilo kufuzu kwenye michuano ya Euro 2024 itakayofanyika baadaye mwaka huu nchini Ujerumani.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 55, hapo awali aliwahi kuwa kocha msaidizi wa Napoli chini ya Maurizio Sarri na Luciano Spalletti.



HABARI MICHEZO

# AZAM YAANIKA SIRI KUIFUNGA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka suluhu dhidi ya Tabora United juzi kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani Tabora, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Azam FC, Thabit Zacharia, amesema moja ya sababu iliyowanyima ushindi kwenye mechi hiyo ni kucheza kwenye jua kali kwani mechi nyingi ambazo timu yao imecheza msimu huu ilikuwa usiku.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoifanya timu hiyo kukwea hadi nafasi ya pili kwa pointi 36 sawa na Simba, lakini ikikaa juu kwa mabao mengi ya kufunga, ikiwa imezidi pia mchezo mmoja, Thabit, maarufu kama Zaka Zakazi, alisema jua kali ni moja kati ya sababu ya kushindwa kuondoka na pointi tatu Tabora.

„Hatukutegemea kupata matokeo haya, lakini tulikuwa tunajua Tabora United wana kikosi kizuri, malengo yetu tulijiandaa kushinda, lakini kwa tahadhari kubwa kwa sababu tulijua tunakuja kukabiliana na timu bora ambayo haipo kwenye nafasi nzuri na unapokutana na timu hii ni hatari sana, tumeathirika na hali ya uwanja haukuwa rafiki, lakini mechi nyingi sisi Azam msimu huu tulikuwa tunacheza usiku, hii tumecheza mchana jua lilikuwa kali sana lilituathiri pia.

Kingine ni baadhi ya wachezaji wetu wametoka kwenye majeraha, hawajakuwa fiti kwa asilimia 100," alisema Zaka Zakazi.

Kocha Youssouph Dabo, alisema baadhi ya wachezaji wake hawakuwa sawa kwenye mchezo huo hasa kwenye maamuzi ya mwisho, lakini pia akilia na majeruhi kikosini mwake ambao ni Prince Dube na Gibrill Sillah.

„Ilikuwa ngumu kwetu, baadhi ya wachezaji wetu hawakuwa sawa leo, hatukuwa na maamuzi mwishoni, inabidi mechi zetu zote tucheze sawa na zingine, tunajisahau kwenye baadhi ya mechi, tuna mechi nyingi mbele lazima tubadilike," alisema Dabo.

Wakati Azam ikifikisha pointi 36, Tabora United ipo nafasi ya 13 na alama zake 17.

HUPITI...




Winga wa kushoto wa Azam FC, Kipre Junior, akimiliki mpira dhidi ya beki wa kulia wa Tabora United, Shaffi Maulid, ambaye anaonekana kuwa makini kuzua hatari hiyo langoni mwake, wakati timu hizo zilipokutana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora juzi na kutoka suluhu. **MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania kuwa mwenyeji CISM

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TANZANIA imepata dhamana ya kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM), utakaofanyika jijini Dar es Salaam Mei 12-19, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mkutano huo, Meja Jenerali wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Francis Mbindi, alisema Tanzania imepata uenyeji wa kuandaa mkutano huu wa 79 ikiwa ni mara ya pili kupata dhamana ambapo mwaka 1991 pia ilikuwa mwenyeji.

Alisema wageni 300 wanatarajiwa kushiriki mkutano huo kutoka nchi wanachama 140 duniani na lengo ni kutumia shughuli za michezo na utimamu wa mwili kama njia ya kueneza amani duniani na tunu za baraza ni kuhamasisha mshikamano, urafiki, heshima, usawa, uadilifu na ushupavu.

Ametaja sababu zilizoibeba Tanzania kuteuliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni uwapo wa amani, ulinzi na usalama.

"Katika mkutano huu ni fursa kutangaza nchi yetu na jeshi letu, lakini pia lugha yetu ya kiswahili itakuwa miongoni mwa lugha tano zitakazotumika kwenye mkutano huu ambapo zingine ni Kiingereza, Kihispania, Kifaransa na Kiarabu," alisema.

Meja Mbindi alisema Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufungua mkutano huo Mei 13, na utafungwa Mei 17, mwaka huu na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

## Yanga tishio nyumbani, Simba

INATOKA UK. 24

Prisons

**Zenye mabao mengi;**
1 – 39 – Yanga
2 – 38 – Azam FC
3 – 31 – Simba SC
4 – 18 – Singida FG
4 – 17 – Prisons

**Zilizofungwa magoli machache**
1 – 08 – Yanga
2 – 11 – Coastal Union
3 – 12 – Azam FC
3 – 12 – Namungo
4 – 14 – Simba

**Zilizofungwa mabao mengi;**
1 – 32 – Mtibwa sugar
2 – 24 – KMC
3 – 22 – Mashujaa FC
4 – 20 – Singida FG, Ihefu
5 – 19 – Prisons, JKT Tanzania

**Zenye sare chache;**
1 – Yanga
2 – Azam FC
2 – Mtibwa Sugar
3 – Simba
4 – Dodoma Jiji, Geita, Ihefu

**Zilizopoteza mechi chache;**
1 – Yanga
1 – Simba
2 – Azam FC
4 – KMC
5 – Coastal, Tabora Utd

**Zilizopoteza mechi nyingi;**
11 – Mtibwa Sugar
09 – Mashujaa FC
08 – Geita Gold
07 – Ihefu, JKT Tanzania
07 – Dodoma Jiji

**Vinara wa mabao;**
10 – Aziz Ki
8 – Maxi Nzengeli
8 – Feisal Salum
8 – Jean Baleke
7 – Prince Dube
7 – Waziri Junior

**Vinara wa asisti;**
6 – Kouassi Yao
6 – Kipre Junior
5 – Impiri Mbombo

## SIMBA KUITIBULIA ASEC REKODI CAF

INATOKA UK. 24

yao ya kufuzu na kwenda kucheza robo fainali ya michuano hiyo.

Katika Kundi B, Asec Mimosas inaongoza ikiwa na pointi 10, Simba ikishika nafasi ya pili kwa alama 5, Jwaneng Galaxy wana alama 4 na Wydad Casablanca wakiburuza mkia katika kundi hilo baada ya kukusanya pointi tatu.

# Michezo

Nipashe

Jumatano Februari 21, 2024


## Mbappe sasa akaribia kumalizana na Madrid

UKURASA 21






# YANGA TISHIO NYUMBANI, SIMBA NI HATARI UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiingia kwenye raundi ya 16, Mabingwa Watetezi na vinara wa ligi hiyo wanaonekana kuwa tishio wakicheza kwenye viwanja vya nyumbani, huku watani zao wa jadi Simba wakionekana hatari zaidi mechi za ugenini.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, Yanga imeshinda mechi zote ilizocheza nyumbani, huku Simba ikiwa haijapoteza mechi yoyote iliyocheza ikicheza ugenini.

Takwimu zinaonyesha kuwa Simba imeshinda mechi saba kati ya nane iliyocheza ugenini, ikitoka sare moja.

Mabingwa Watetezi, Yanga wameshinda mechi zote nane walizocheza wakitumia uwanja wao wa nyumbani. Walicheza mechi ya kwanza nyumbani Agosti 23, mwaka jana, wakaitwanga KMC mabao 5-0, kabla ya kushinda tena idadi hiyo ya mabao dhidi ya JKT Tanzania, Agosti 29, na wakashinda bao 1-0 dhidi ya Namungo wakiwa nyumbani, ambapo mechi zote hizo walitumia Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Yanga iliendeleza vipigo ikicheza viwanja vyake vya nyumbani Oktoba 23, mwaka jana ilipoifumua Azam FC mabao 3-2, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Oktoba 27 ikaifunga Singida Fountain Gate mabao 2-0, ikaisasambua Mtibwa Sugar mabao 4-1, Desemba 16, mwaka jana, na mwaka huu, Februari 5, iliidungua Dodoma Jiji bao 1-0, kabla ya kuiadhibu Mashujaa FC mabao 2-1.

Ilipomaliza kucheza dhidi ya Azam FC, Yanga ilendelea kuutumia Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kama wake wa nyumbani. Ikicheza ugenini, Yanga imecheza pia mechi nane, lakini ikishinda sita, sare moja na kupoteza mechi moja.

Imevuna pointi 24 ikicheza mechi za nyumbani, na 19 ikicheza viwanja vya ugenini.

Simba, ikicheza ugenini, iliifumua Mtibwa Sugar mabao 4-2, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani Morogoro, Agosti 17, mwaka jana, iakaenda Uwanja wa Sokoine Mbeya na kuachia kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Prisons, mechi iliyochezwa Oktoba 5, mwaka jana, ikaifunga Singida Fountain Gate mabao 2-1, Uwanja wa Liti, Singida, Oktoba 8 na kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC, Desemba 23, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Iliendeleaa rekodi yake nzuri ya viwanja vya ugenini msimu huu kwa kuisulubu Mashujaa FC mabao 2-1, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, Februari 3, mwaka huu na Februari 6 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ilitoa kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya Tabora United.

Kama vile haitoshi, iliidungua Geita Gold bao 1-0, Februari 12, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza na kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam iliichapa JKT Tanzania bao 1-0.

Ikicheza uwanja wake wa nyumbani, Simba imecheza mechi saba, ikishinda nne, sare mbili ikivuna pointi 14 nyumbani, huku kwenye viwanja vya ugenini ikizoa pointi 22, kwa kushinda mechi saba na sare moja.

**Baadhi ya takwimu hadi sasa**

**Vinara wa pointi;**

1 – 43 – Yanga
2 – 36 – Azam FC
3 – 36 – Simba
4 – 23 – Coastal Union
5 – 22 – KMC

**Zilizoshinda mechi nyingi;**

1 – 14 – Yanga
2 – 11 – Azam FC
3 – 11 – Simba
4 – 06 – Coastal Union
5 – 05 – KMC, Singida FG,

INAENDELEA UK. 23

## Simba kuitibulia Asec rekodi CAF

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikitua salama Ivory Coast tayari kwa mchezo wao wa raundi ya tano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola, ametamba kuwa wamekwenda nchini humo kwa kazi mbili, kushinda mechi na kujiweka katika mazingira mazuri ya kutinga hatua ya robo fainali, lakini kutibua rekodi ya wapinzani wao ambao hawajapoteza mechi yoyote kwenye Kundi B.

Simba iliondoka na wachezaji 22 usiku wa kumkia jana kuelekea nchini humo ikiwa na lengo la kuhakikisha inapata ushindi katika mchezo huo, na moja kati ya walichokiangalia zaidi ni kutoruhusu bao katika mchezo huo utakaochezwa uwanja wa Felix, Houphouel-Boign, Ijumaa wiki hii.

Akizungumza na Nipashe, Matola alisema benchi la ufundi na wachezaji wanatambua ugumu wa mechi hiyo na wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kupambania timu kupata matokeo chanya.

Alisema Asec Mimosas inataka kupata rekodi nzuri katika michuano hiyo kwa kuongoza kundi hilo, lakini wamejiandaa kutibua rekodi hiyo kwa kutoruhusu kufungwa katika mchezo huo na kutumia nafasi zinazopatikana.

"Tumewaangalia Asec Mimosas hivi karibuni tunaenda kucheza na timu ngumu, ikitaka kuendeleza rekodi yake, lakini kwa upande wetu tumejipanga vizuri safu ya ulinzi kuwa makini na washambulia wa wapinzani huku wetu tukiwapa jukumu la kuhakikisha tunavuna alama muhimu katika mchezo huo.

"Kurejea kwa beki wetu, Henock Inonga ni jambo zuri kwa sababu anazidi kuimarisha safu ya ulinzi kwa kutibua mipango yao na kupambana kutafuta pointi ugenini na kuja kushinda katika mechi yetu ya nyumbani dhidi ya Jwaneng Galaxy," alisema Matola.

Aliongeza kuwa wakifanikiwa kupata alama dhidi ya Asec Mimosas na kushinda mechi yao ya nyumbani, watafikia malengo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >

Gamondi